# KCSE 2024 REGIONAL MOCKS

# KISWAHILI

***The PDF Comprises of A Compilation of 4 Top Joint National Mocks Administered across the 47 Counties for KCSE Class of November 2024***

**For Marking Schemes:**

**Call/ Text/ Whatsapp 0724333200/0795491185/ 0768321553**

***Mr Machuki***

**Or**

**Visit or website**

**www.kenyaeducators.co.ke**

**KENYA EDUCATORS CONSULTANCY**

# *Table of Contents*


| | |
|---|---|
| **1.** | **Nairobi & Central Joint National mocks 2024** |
| **2.** | **Nyanza & Western Joint National mocks 2024** |
| **3.** | **Coastal & Eastern Joint National mocks 2024** |
| **4.** | **Rift Valley & North Eastern Joint National mocks 2024** |


**Confidential!!!**

***Success to all KCSE 2024 Candidates***

# KENYA EDUCATORS CONSULTANCY

**JINA**.............................................................................................**NAMABARI**............................

**SHULE**.........................................................................................**TAREHE**.................................

**DARASA**...............................................................................**SAHIHI**.........................................

**102/1**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 1**
**CLASS OF KCSE 2024**
**TIME: 2 HOURS**

# THE NAIROBI & CENTRAL REGIONS KCSE JOINT NATIONAL MOCK 2024

***Kenya Certificate of Secondary Education (KCSE)***

**MAAGIZO KWA MTAHINIWA:**

1) Andika jina lako, nambari ya mtihani na tarehe katika karatasi ya majibu.
2) Karatasi hii ina maswali manne.
3) Jibu maswali mawili pekee. Kila swali lina alama ishirini.
4) Swali la kwanza ni la lazima.
5) Chagua swali jingine lolote kutoka kwa matatu yaliyosalia.
6) Majibu yote yaandikwe katika karatasi ya majibu uliyopewa.
7) Majibu yote yaandikwe katika lugha ya Kiswahili.

***Sehemu hii imehifadhiwa kwa matumizi ya mtahini pekee.***

| **SWALI** | **1** | **2** | **3** | **4** |
|---|---|---|---|---|
| **UPEO** | **20** | **20** | **20** | **20** |
| **ALAMA** | | | | |

**JUMLA**

| | |
|---|---|
| **UPEO** | **40** |
| **ALAMA ZA MTAHINIWA** | |

***©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]***

1. Wewe ni Waziri wa Elimu nchini mwako. Wizi wa Mitihani ya Kitaifa umekuwa janga kuu. Andika hotuba utakayoitoa mbele ya washikadau wa elimu ili kudhibiti janga hili.
2. Ajali za barabarani ndizo chanzo cha vifo vingi nchini. Janga hili limekuwa tatizo sugu kulingana na Waziri wa Usalama. Eleza vyanzo mbalimbali vya ajali hizi.
3. Simulia kisa cha kusisimua kuthibitisha ukweli wa methali: Ajuaye misonoe ni alalaye naye.
4. Tunga kisa kitakachoisha kwa maneno yafuatayo:
   ... niliyasikiliza maneno yake kwa uchungu kwa kuwa nilielewa fika kwamba maji yakimwagika hayazoleki.

***©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]***

**JINA.......................................................................................................NAMABARI...............................**

**SHULE....................................................................................................TAREHE...................................**

**DARASA.........................................................................................SAHIHI..........................................**

**102/2**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 2**
**CLASS OF KCSE 2024**
**TIME: 2 HOURS**

# THE NAIROBI & CENTRAL REGIONS KCSE JOINT NATIONAL MOCK 2024

***Kenya Certificate of Secondary Education (KCSE)***

**Maagizo**

a) Andika jina lako na nambari yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
b) Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
c) Jibu maswali **yote**.
d) Majibu yote yaandikwe kwa nafasi ulizoachiwa.
e) Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya **Kiswahili**.

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| Ufahamu | 15 | |
| Ufupisho | 15 | |
| Matumizi ya lugha | 40 | |
| Isimujamii | 10 | |
| JUMLA | 80 | |

*©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]*

**Sehemu A: UFAHAMU (Alama 15)**

**Soma kifungu kifuatacho kasha ujibu maswali uliyopewa.**

Kwa miaka mingi, maafisa wa afya ya jamii wamekuwa wakitahadharisha umma kuhusu athari za moshi wa sigara. Sasa kwa mara ya kwanza, watafiti wanasema wamethibitisha moshi wa sigara ni hatari kwa wasiovuta sigara.

Aidha wanasayansi hao wanasema moshi wa sigara husababisha mabadiliko makubwa katika mapafu ya mtu asiyevuta sigara. 'Tumesikia kwa muda mrefu kwamba moshi wa sigara ni hatari kwa afya ya watu wasiovuta sigara lakini sasa tumepata thibitisho. Kwa mara ya kwanza, tumefanikiwa kutazama uharibifu wa moshi wa sigara kwa mapafu ya wahusika,'' watafiti hao walisema katika ripoti yao iliyochapishwa mnamo mei 20 katika jarida moja la kisayansi.

Katika utafiti wao, watafiti hao walifanyia uchunguzi mapafu ya watu ambao hawakuwa wakivuta sigara japo walikuwa wakiishi na jamaa au marafiki waliokuwa wakivuta sigara. Aidha, watafiti hao waligundua kwamba mapafu ya thuluthi moja ya watu hao waliofanyiwa utafiti yalikuwa yameharibiwa vibaya sana kutokana  na moshi wa sigara.

Ilithibitishwa kuwa mapafu ya watu hao ambao hawakuwa wakivuta sigara yalikuwa sawa na ya wale ambao walikuwa wakivuta sigara. Kwa hivyo, mtu yeyote anayevuta sigara anapaswa kujua anaathiri yule aliye karibu na yeye. Watu ambao hawavuti sigara na ambao wanakaa karibu na wale wanaovuta sigara wamo katika hatari kubwa ya kuugua magonjwa mbalimbali yanayohusiana na moshi wa sigara. Kwa mujibu wa maafisa wa afya, moshi wa sigara unaweza kusababisha magonjwa ya pumu, masikio na nimonia miongoni mwa watu wasiovuta sigara. Moshi wa sigara kadhalika unaweza kusababisha vifo miongoni mwa watoto wachanga.

Isitoshe, moshi wa sigara ni hatari kwa watu wazima wasiovuta sigara kwa sababu unaweza kuwaweka katika hatari kubwa ya kuugua magonjwa hatari ya kansa ya mapafu, moyo na damu na mshutuko wa moyo. Watu ambao hawavuti sigara wanashauriwa dhidi ya kukaa karibu na watu wanaovuta sigara au kuwakubali watu kuvuta sigara ndani ya nyumba zao. Mtu anayekaa karibu na mtu anayevuta sigara hata dakika 8 hadi 20 yumo katika hatari kubwa ya kuugua magonjwa ya moyo na shida mbalimbali za kupumua.

Kadhalika, wanawake wajawazito wanaokaa karibu na wavutaji sigara au wanaoishi na wavutaji sigara wamo hatarini ya kuzaa watoto walio na uzito wa chini mno. Kadhalika ni rahisi kwa mimba yao kuharibika.

*©KNEC 2024  [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]*

Watoto wachanga ndio wamo hatarini kubwa ya kukumbwa na magonjwa hayo kwa sababu mapafu yao bado ni machanga mno kuweza kuhimili athari za moshi wa sigara

**Maswali:**

**a)** Andika kichwa mwafaka cha kifungu ulichosoma. (alama 2)

………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………

**b)** Taja vikundi viwili vinavyoathiriwa na sigara.(alama 2)

………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………

**c)** Ni magonjwa yapi yanayoweza kusababishwa na moshi wa sigara? (alama 5)

………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………

**d)** Eleza matokeo ya utafiti uliofanyika. (alama 2)

………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………

**e)** Ni nini maoni ya mwandishi? (alama 2)

………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………

***©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]***

**f)** Taja vikundi viwili vinavyoathirika sana na uvutaji sigara. (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………

**SEHEMU B: MUHTASARI**

Uhuru wa Sudan Kusini.

Imewachukua wananchi wa sudan kusini muda wa miaka 56 kujitawala. Vita vya kupigania uhuru vilianza mnamo mwaka wa 1953. Kuna sababu kadhaa zilizosababisha wananchi wa Sudan kusini kupigana. Miongoni mwake ni rasilimali ya mafuta ambayo hupatikana upande wa Kusini japo haikuwa inawanufaisha kwa lolote. Mafuta haya yakiuzwa pesa zilizopatikana zilikuwa zinaendeleza upande wa Kaskazini pekee. Pia kulikuwa na ubaguzi wa rangi ambapo watu weusi wa upande wa Kaskazini, Watu wa Kusini walilazimika kujifunza lugha ya Kaskazini ambayo ni Kiarabu. Pasi na kuijua lugha hii, raia wa Kusini hawangepata kazi kule kaskazini.

Isitoshe, hakuna maendeleo yoyote upande wa Kusini. Miundomsingi ni mibaya na hakuna shule wala chochote kinachodhihirisha maendeleo. Upande wa juu uliongozwa na sheria za Uislamu, maarufu kama Sharia. Upande wa Kusini una Ukristo, jambo ambalo lilizua uhasama mkubwa wa kidini. Watu wa Kusini walihisi wamebaguliwa sana kwa msingi ya kidini.

Shujaa John Garang ni miongoni mwa Wasudani wa Kusini ambao walileta kugawanywa kwa nchi ya Sudan ili watu weusi wajitenge na waarabu. Alipofariki mnamo mwaka 2006, alikuwa ameiongoza Sudan ya Kusini kuweka mkataba na Sudan ya Kaskazini kuhususiana na nchi kushiriki katika kura ya maamuzi.

Japo kabla ya hii kura kupigwa, wananchi wa Sudan wanamheshimu sana kwa mchango wake kwenye mkutano uliokuwa Naivasha na ambao uliwapa wananchi wa Sudan Kusini kuamua iwapo walitaka kujitawala au la. Kura hii ilipigwa mnamo mwezi wa Disemba 2010. Sasa taifa hili ni huru.

Rais wa sasa wa Sudan Kusini, Bw. Salva Kiir anatarajiwa kuongoza taifa hili changa ili kufikia maendeleo makubwa. Hana budi kushirikiana na mataifa ya ulimwengu ili yamsaidie katika kuyatimiza malengo yake.

Sisi kama wakenya tutanufaika si haba. Tayari benki za hapa nchini kama Equity na KCB zina matawi yake huko. Isitoshe, tayari wafanyabiashara wetu wamepenya mpaka huko na biashara ya kuuza nafaka na bidhaa nyingine imenoga sana. Japo safari ya kutoka Nairobi mpaka

***©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]***

Juba ni ndefu na yenye hatari, malipo yake ni mazuri. Isitoshe katika juhudi za kulijenga taifa hili changa, pana uwezekano kuwa Wakenya watapata nafasi za kazi. Hivyo wale amabo wamesoma wananufaika si haba. Pia hazina yao kubwa ya mafuta itatufaidi kwa maana tunaweza kununua kutoka kwao kuliko kuyaagiza kutoka nchi za Uarabuni.

Kadhalika, wakimbizi kutoka humo sasa wamerudi kwao na hivyo mzigo mkubwa wa wakimbizi umepungua kidogo. Wakiipata amani, nasi pia tutaipata na hatutakuwa na vita tena mipakani. Utangamano pia utakuwepo hasa kwenye miji ya mipakani. Licha ya manufaa haya yote, hivi karibuni mwaka wa 2013, Disemba; Sudan Kusini imerudi tena katika vita vya wenyewe kwa wenyewe kati ya serikali ya Riek Machar. Hali hii imeleta wasiwasi duniani kuhusu hatima ya taifa changa la Sudani Kusini. Hata hivyo, bado kuna matumaini ya kurudia amani kwani juhudi za upatanishi zinafanywa na Umoja wa Africa(AU).

<u>MASWALI</u>

a) Kwa nini wananchi wa sudan kusini walipigania uhuru wao ?(maneno 30-35) (alama 6,1 ya mtiririko)

Matayarisho

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………

Jibu/nakala safi

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………

b) Sisi kama wakenya tutafaidika vipi taifa hili la Sudan Kusini litakapojitawala?(maneno 50)alama 9;2 mtiririko matayarisho nakala chafu)

Matayarisho

……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………

Jibu/nakala safi

……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………

***©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]***

**MATUMIZI YA LUGHA(ALAMA 40**)

a) Tunga sentensi zenye viambishi awali vifuatavyo
   i. Kukanusha wakati (alama 2)

   ii. Kirejeshi

b) Tumia kiambishi –ki-katika sentensi kuonyesha (alama 1)
   i. Waktai ujao hali ya kuendeleza

   ii. Hali timilifu katika wakati wa kuendelea.

c) Huku ukitumia viambishi u na ji unda nomino kutokana na vitenzi hivi. (alama 1)
   i. Zungumza

   ii. Kwea

d) Kanusha sentensihizi (alama 2)
   i. Kuliko na vita ni kule kulichochewa na wanasiasa

   ii. Kanusha sentensi hii kwa kuzingatia sehemu iliyopigiwa mstari.

   Utakapokuwa mkubwa utayaelewa mambo haya.

***©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]***

e) Yape maneno haya ngeli zao(alama 2)
   i. Ghubari-
   ii. Gulio-

f) Vifungie sentensi viunganishi hivi(alama 1)
   i. Mingairi ya
   ii. Fakaifa

g) Ikamilishe methali hii kisha uitolee maana na matumizi(alama 3)
   Mlenga jiwe  kundini…………………………

h) Tunga sentensi kudhihirisha maana ya maneno haya (alama 1)
   i. Nyange
   ii. Kulungu

i) Unda jina kutokana na neno hili. (alama 1)
   i. Husudu
   ii. Ashiki

j) Tumia'vua'kama. (alama 2)
   i. Kishazi huru
   ii. Kishazi tegemezi

***©KNEC 2024  [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]***

k) Taja sifa mbili bainifu za sauti/d/(alama 2)

i. …..
ii. ……
iii. …….

l) Eleza matumizi ya 'kwa' katika sentensi zifuatazo.(alama 2)

i. Vijana kwa wazee walikusanyika ukumbini

ii. Kakake alifanya kazi hiyo kwa ufasaha.

m) Onkwani: mama!ulinipata wapi mimi?
Mama: nilikuzaa,onkwani.
Andika upya katika usemi wa taarifa ambapo mama Onkwani anamweleza baba Onkwani kuhusu mazungumzo haya.(alama 4)

n) Tofautisha matumizi ya 'po' katika sentensi ifuatayo;-
Talanta alipokuwa safarini kwenda Mombasa aliona palipoanguka gari lililokuwa limebeba mahindi.(alama4)

o) Unganisha sentensi hii kwa kutumia kirejeshi cha kati (alama 2)
Wavu umekatika. Wavu ni wao.

p) Andikja wingi wa sentensi hii katika hali ya ukubwa(alama 2)
Kigoma chake kilipigwa hadi kikapasuka

***©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]***

q) Twasema;(alama 2)
Kiatu cha mwanafunzi kimepotea.
Toa kiatu na badala yake tumia kaniki

r) Tofautisha sentensi hizi (alama 2)

i. Ningalimwona jana ningalifurahi.

ii. Ningemwona jana ningefurahi

s) Onyesha aina za shamirisho katika sentensi hizi(alama 3)

i. Mama alipika wali

ii. Moishi alikatakata nyama kwa kisu.

iii. Kasisi aliwahubiria waumini kanisani

t) Tunga sentensi kuonyesha viwakilishi hivi(alama 1)

i. A-unganifu,ngeli ya LI-YA umoja

ii. Viwakilishi vya sifa,ngeli ya U-I wingi.

## ISIMU JAMII (ALAMA 10)

"Toa zote mpaka senti ya mwisho! Unanisikia, chapuchapu au nikuset.

a. Hii ni sajili gani? Toa sababu.(alama 2)

b. Eleza sifa tatu za sajili hii(alama 3)

c. Eleza maana ya msamiati ufuatao kama unavyotumiwa katika isimu jamii.(alama 10)

   i. Lahaja

   ii. Ujozi lugha

   iii. Wingi lugha

***©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]***

iv. Krioli

v. pijini

**JINA................................................................................................NAMABARI............................**

**SHULE.................................................................................................TAREHE..................................**

**DARASA.........................................................................................SAHIHI..........................................**

**102/3**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 3**
**CLASS OF KCSE 2024**
**TIME: 2 HOURS**

# THE NAIROBI & CENTRAL REGIONS KCSE JOINT NATIONAL MOCK 2024

***Kenya Certificate of Secondary Education (KCSE)***

**MAAGIZO**

a) Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu
b) Jibu maswali manne pekee
c) Swali la kwanza ni la lazima
d) Maswali hayo mengine yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobakia yaani : Riwaya, hadithi fupi,ushairi na fasihi simulizi
e) Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja
f) Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili
g) Majibu yote sharti yaandikwe kwenye nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| USHAIRI | 20 | |
| TAMTHILIA | 20 | |
| RIWAYA | 20 | |
| HADITHI FUPI | 20 | |
| FASIHI SIMULIZI | 20 | |
| JUMLA | | |

*©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]*

**SEHEMU A: TAMTHILIA**

**Timothy M.Arege :Bembea ya Maisha**

1. **LAZIMA**

La! Kila mbegu ipandwayo haina budi kuzaa na izaapo mazao yake huvunwa. Mtu hutakasa sahani akijua itamfaa tena. Kinacholelewa hakina budi kulea.

a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama4)

b) Changanua mtindo katika dondoo hili (alama3)

c) Kauli iliyopigiwa mstari inaonyesha majukumu ya watoto kwa wazazi. Thibitisha kwa kuonyesha wazi alivyowajibika anayerejelewa na msemaji (alama4)

d) Fafanua umuhimu wa msemaji katika kujenga tamthilia ya Bembea ya Maisha (alama4)

e) Eleza sifa tano za msemewa (alama5)

**SEHEMU B: RIWAYA**

**A. NGUU ZA JADI**

**Jibu swali la 2 au la 3**

2. . Fafanua matumizi ya hadithi ndani ya hadithi katika kukuza vipengele vifuatavyo:
(i)Maudhui

(ii)Wahusika

Rejelea:

Kisa cha Lilith (uk.81-82)

(i) Jinsi kinakuza maudhui (al.10)

(ii) Jinsi kinakuza wahusika(al.10)

3. Kisa cha kijana mmoja ambaye aliugua ugonjwa wa Pediculosis orporis(uk.131-132)

i) Jinsi kinakuza maudhui(al.10)

(ii) Jinsi kinakuza wahusika(al.10)

(iii)Jinsi kinakuza maudhui(al.10)

(iv) Jinsi kinakuza wahusika(al.10)

**SEHEMU C:HADITHI FUPI**

**MAPAMBAZUKO YA MACHWEO NA HADITHI NYINGINE**

***©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]***

**Jibu swali la 4 au la 5**

Racheal Wangare:Fadhili za Punda

"Rudi, nyumbani mwanamke wewe! Nitakuja jioni tuyamalize haya."

a)(i) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama4)

(ii) Fafanua hulka ya msemaji wa kauli hii (alama4)

iii) Huku ukizingatia hadithi hii, jadili maudhui ya mabadiliko yanavyojitokeza katika hadithi(alama7)

b) Changanua mtindo katika dondoo hili (alama 5)

Alasiri ile, baada ya ibada mbili, mhubiri akawa hoi kwa mavune. Akatamani kufika nyumbani apumzike, kazi ya kuwalisha kondoo wa Mungu si kazi rahisi. Wamefika nusu safari, bintiye katulia kama maji ya mtungi. Akimtazama kipembe anamkumbusha marehemu mkewe. Miaka mitatu sasa na dhiki ya kuondokewa haijamwisha. Alihisi ukiwa, akatamani mwenziye. Sasa kazi kukilea kitoto chao, kibinti hiiki kilicho mlanda mamake kama shilingi kwa ya pili. Nyuma ilijaa kicheko alipokua hai mamake. Kama si bintiye ambaye ulimi wake hautulii, kiroho kingemvamia labda hata kumvuta kuelekea kaburini .

AU

5. Winnie Nyaruri Ogenche; Sabina

"Ninaomba wazazi wenzangu muwape watoto wa kike elimu badala ya kuwaoza mapema. Hongera, mwanangu kwa kupata alama mia nne arubaini na saba"

a) Eleza umuhimu wa mrejelewa katika kukuza hadithi husika (alama5)

b) Tambua mbinu ya kimtindo iliyotumika katika dondoo hili (alama1)

c) Fafanua jinsi mbinu yenyewe ilivyotumika ili kufanikisha utunzi wa hadithi (alama6)

d) Fafanua changamoto zinazokabili jinsia ya kike kwa mujibu wa hadithi (alama8)

**SEHEMU D :USHAIRI**

**Jibu swali la 6 au la 7**

Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali

Nazuka mtunga mambo, na watunzi watungao
**Wafungatao masombo,** kushika msu na ngao
Naipiga ya ngambo, sauti ifike kwao
Wawapi wajigambao, tugambiyane vigambo?

Ni siku nyingi kitambo, **ninyemele** naja leo
Kama kweli wana nyimbo, nawaje niimbe nao
Na sababu ni vigambo, vya wale wajitwazao
Wawapi wajigambao,tugambiyane vigambo?

Iwapo mu wana nyimbo, na ungoi upasao
Musingewaonya mambo, waoga mwatishao

*©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]*

Mungefungata masombo, kuteta na wawezao
Wawapi wajigamboa, tugambiayane vigambo?

Wawapi fundi wa nyimbo, malengo wajitwazao
Wasemao kula jambo, kuwa walijua wao
Kuna kipambua pambo, chatafuta wapambao
Wawapi wajigambao,tugambiyane vigambo?

Musidhani ni msimbo, hayano nambano leo
Nawaeleza ni mambo, yamtaka atakao
Ajifungate msombo,mdudoateze nayo
Wawapi wajigambao, tugambiyane vigambo?

Imani wenya utambo, mutambao kwa matao
Muelewao mafumbo, na mbinu za wafumbao
Kuna 'tomvu za ulimbo, tengani muruke nao
Wawapi wajigambao, tugambiyane vigambo?

Sasa tafunuwa wimbo, takasani masikio
Siimbi la mtu jambo, alojiweka kituo
Hili' metunga no fumbo, n' nao niwatakao
Wawapi wajigambao, tugambiyane vigambo?

Tamati enyi warembo, nasubiri matokeo
Hivi sasa sina jambo, ela naaga nendao
Ni mimi simba wa wimbo,marara ningurumao
Wawapi wajingambao, tugambiyane vigambo?

Maswali

a) Lipe shairi hili anwani mwafaka (alama1)
b) Eleza muundo wa shairi hili (alama4)
c) Taja na utoe mifano ya mbinu nne za kimtindo zilizotumika katika shairi hili (alama4)
d) Fafanua uhuru wa kishairi katika ubeti wa nne (alama3)
e) Andika ubeti wa pili katika lugha ya nathari (alama4)
f) Tambua nafsi nenewa katika shairi hili ` (alama1)
g) Taja toni la shairi hili (alama1)
h) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika ushairi (alama2)
   i) Wafungatao masombo
   ii) Ninyemele

©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]

7. **Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali:**

Binadamu hatosheki, ni kiumbe chenye zani, kweli mja hapendeki,
Kwa kweli haaminiki, hila ameficha ndani, la wazi ni unafiki
Ukweliwe haafiki, njama zake zi moyoni, usimwone ni rafiki
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka,

Wengine watakuua, wakiona una pesa, hata zikiwa kidogo,
Hizo kwao ni maua, hupupiwa zikatesa, wakazifuata nyago,
Hadi kwenye wako ua, pasipo hata kupesa, wala kukupa kisogo,
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka

Pindi kinunua kitu, hafurahi Shaitani, bali tajawa chukizo,
Mtu kiwa mtukutu, tanuna mtimani, kwalo lako tekelezo,
Tamko lake 'Subutu' Kuondoa tumaini, na kukuulia wazo,
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka,

Aliye na taraghani, taabu kuishi naye, kazi yake kujidai,
Takusema faraghani, asosema kiwa naye, kupendeza maadui,
Hana faida nyumbani,ni mtu akuchimbaye, mradi usitumai,
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka,

Kwa hakika ni balaa, kumkirimu mchawi, aliyejaa uchoyo,
Bahati ina hadaa, kukupa alo sadawi, aibatili rohoyo,
Mipangoyo kwake jaa, na nia ya ustawi, huwiza kuvunja kaninyo,
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka.

Ninacho changu kilio, ninalia sanasana, kinyesi nimetupiwa,
Ningetoa azimio, lakini uwezo sina, kwa matatizo kuambiwa,
Ama nitumie mbio, fuadini ninanena, akilini nazuiwa,
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka.

**MASWALI:**

a) Lipe shairi hili anwani mwafaka (alama1)

b) Fafanua mambo **manne** mabayo nafsineni analalamikia (alama4)

c) Ainisha shairi hili kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo: (alama3)
(i) Idadi ya vipande katika kila mshororo
(ii) Mpangilio wa vina katika kila ubeti
(iii) Idadi ya mishororo katika kila ubeti

d) Andika ubeti wa **nne** katika lugha nathari (alama3)

***©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]***

e) Bainisha tamathali **mbili** za usemi zilizotumiwa katika shairi hili (alama2)

f) Huku ukitoa mifano, onyesha mbinu **mbili** alizotumia mshairi kutosheleza mahitaji ya kiarudhi (alama2)

g) Andika aina **mbili** za urudiaji zilizotumiwa katika shairi hili (alama2)

h) Fafanua muundo wa ubeti wa **tano** na **sita** (alama3)

**SEHEMU E : FASIHI SIMULIZI**

8 .Niaje wazungu wanaweza kutunza vitu vikajaa kwenye friji. Yani nimeweka soda mbili tu kweye friji lakini akili haitulii hadi nizinywe. Niko sebuleni nazunguka tu. Najaribu kuwaza vitu vingine lakini wapi akili inaniambia ‘My friend, kunywa soda.’

a) Bainisha kipera cha utungo huu (alama1)

b) Fafanua aina tatu za taswira zilizotumika katika kifungu hiki (alama3)

c) Utanzu wa kipera hiki huweza kuchukua nafasi muhimu katika fasihi simulizi. Thibitisha kwa hoja zozote sita (alama6)

d) Ufanisi wa uwasilishaji wa utanzu huu unategemea fanani. Teteta kauli hii. (alama5)

e) Ni changamoto zipi zinaweza kumkabili mwanafasihi mtafiti nyanjani? (alama5)

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]

*©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at [www.kenyaeducators.co.ke](http://www.kenyaeducators.co.ke)]*

©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]

*©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at [www.kenyaeducators.co.ke](http://www.kenyaeducators.co.ke)]*

..............................................................................................................................................................

..............................................................................................................................................................

..............................................................................................................................................................

..............................................................................................................................................................

..............................................................................................................................................................

..............................................................................................................................................................

..............................................................................................................................................................

..............................................................................................................................................................

..............................................................................................................................................................

..............................................................................................................................................................

..............................................................................................................................................................

..............................................................................................................................................................

**HII NDIO UKURASA WA MWISHO KUPIGWA CHAPA!**

*©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]*

**JINA.........................................................................................NAMABARI............................**

**SHULE.....................................................................................TAREHE..................................**

**DARASA...........................................................................SAHIHI.........................................**

**102/1**

**KISWAHILI**

**KARATASI YA 1**

**CLASS OF KCSE 2024**

**TIME: 2 ½ Hours**

# THE NYANZA & WESTERN REGIONS KCSE JOINT NATIONAL MOCK 2024

***Kenya Certificate of Secondary Education (KCSE)***

**MAAGIZO KWA MTAHINIWA:**

1) Andika jina lako, nambari ya mtihani na tarehe katika karatasi ya majibu.
2) Karatasi hii ina maswali manne.
3) Jibu maswali mawili pekee. Kila swali lina alama ishirini.
4) Swali la kwanza ni la lazima.
5) Chagua swali jingine lolote kutoka kwa matatu yaliyosalia.
6) Majibu yote yaandikwe katika karatasi ya majibu uliyopewa.
7) Majibu yote yaandikwe katika lugha ya Kiswahili.

***Sehemu hii imehifadhiwa kwa matumizi ya mtahini pekee.***

| **SWALI** | **1** | **2** | **3** | **4** |
|---|---|---|---|---|
| **UPEO** | **20** | **20** | **20** | **20** |
| **ALAMA** | | | | |

**JUMLA**

| | |
|---|---|
| **UPEO** | **40** |
| **ALAMA ZA MTAHINIWA** | |

***©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]***

1. Ndugu yako ameamua kuasi ukapera. Andika ratiba itakayotumiwa siku ya arusi yake.
2. Eleza mikakati ambayo serikali ya Kenya imeweka kukabiliana na mashambulizi ya mara kwa mara ya Kigaidi nchini.
3. Andika insha kuonyesha busara iliyomo katika methali "Mchelea mwana kulia hulia mwenyewe".

4. Andika insha itakayomalizika kwa maneno haya:

   ……………Nilikumbuka ushauri niliopewa na mama mazazi mara kwa mara. Uchungu usiomithilika ulinichoma moyoni, laiti ningalijua.

*©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]*

**JINA.........................................................................................NAMABARI.............................**

**SHULE.......................................................................................TAREHE..................................**

**DARASA...........................................................................SAHIHI.........................................**

**102/2**

**KISWAHILI**

**KARATASI YA 2**

**CLASS OF KCSE 2024**

**TIME: 2 ½ Hours**

# THE NYANZA & WESTERN REGIONS KCSE JOINT NATIONAL MOCK 2024

***Kenya Certificate of Secondary Education (KCSE)***

**Maagizo**

a) Andika jina lako na nambari yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
b) Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
c) Jibu maswali **yote**.
d) Majibu yote yaandikwe kwa nafasi ulizoachiwa.
e) Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya **Kiswahili**.

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| **Ufahamu** | **15** | |
| **Ufupisho** | **15** | |
| **Matumizi ya lugha** | **40** | |
| **Isimujamii** | **10** | |

*©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]*

| | | |
|---|---|---|
| **JUMLA** | **80** | |

1. **UFAHAMU** **ALAMA 15**

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata.*

Seneta maalum kutoka Mombasa, Bi. Miraj Abdillah aliwasilisha mswada bungeni wenye nia ya kuwawezesha watoto wasichana wanaotungishwa mimba wakiwa shuleni kuwa na uwezo wa kukamilisha elimu yao. Kulingana naye, maisha ya wasichana wengi hufikia kikomo pindi tu wanapojipata katika hali hii, inayowafanya kuwa wazazi kabla ya wao kuwa tayari. Kwa sasa msichana anapojipata katika hali hii, kuna uwezekano wa kutorejea shuleni hata ingawa wizara ya elimu ina sera inayowataka walimu kutowafukuza.

Pendekezo la Bi. Miraj linaashiria kuwa wasichana wa eneo la pwani na nchi nzima hawafai kuhangaishwa na walimu wanapotafuta nafasi ya kuendeleza masomo yao baada ya kujifungua. Japo pendekezo hilo ni nzuri, kuna mambo kadhaa muhimu ambayo huenda yakitekelezwa yatawasaidia wasichana hao kurejelea maisha yao ya kawaida. Wengi wao katika eneo la pwani wanapojifungua huwa wanalazimika kuwaachia watoto au walezi wao watoto waliozaliwa ili nao waweze kuhudhuria masomo yao.

Licha ya hayo, wengine hulazimika kuondoka shuleni ili kuwashughulikia watoto wao ambao ni wachanga hasaa wale ambao bado ni wachanga na wanaotegemea maziwa ya mama. Huku mswada huo ukiandaliwa, kuna umuhimu wa kuchunguza jinsi ya kuwakubalia akina mama hao wachanga, kuondoka shuleni mapema au hata kuletewa watoto wao shuleni wawanyonyeshe. Hili likifanyika ina maana kuwa angaa chumba maalumu cha kuwashughulikia watoto wao kitafaa zaidi.

Serikali za Kaunti pia zinaweza kutenga kiwango cha fedha cha kuwasaidia wasichana hawa kukidhi watoto wao ili muda ambao wangetumia kwenda kutafuta tonge wautumie kusoma. Mara nyingi wengine huamua kuacha shule ili wawashughulikie wanao. Mbali na hilo serikali pia inapaswa iandae hamasisho katika shule na hata vijijini kuhusu suala la wasichana kuendelea na masomo yao.

Kuwa na sheria pekee huenda kukakosa kuweka mazingira mazuri ya wasichana hao kurejea shuleni. Mfano mzuri ni wa kejeli atakazokutana nazo msichana yule, atakapokuwa akisoma kabla ya kujifungua na hata baada ya kujifungua. Kuna umuhimu wa wanafunzi wa wanafunzi

***©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]***

shuleni kuhamasishwa kuwa mambo haya hutokea. Kuelezwa kuwa mmoja wao ajipatapo katika hali hiyo si nafasi ya kumkejeli, huenda kukazua mazingira mazuri kwao wanapoendelea na masomo.

Isitoshe, kuna pia umuhimu wa kuwepo na washauri wazuri wa kuwahimiza akina mama hao wachanga kuwa bado wana nafasi. Kuwa tu na sheria huenda kukawapa ugumu wasichana hawa kurejea darasani. Hivyo basi, pendekezo la Seneta Maalum ni zuri sana, ila kuna umuhimu wa mashirika, jamii na hata serikali kuangalia suala hili kwa zaidi ya misingi ya sera tu. Ni aula kuhakikisha kuna mazingira mwafaka kwa wasichana hao wanapokuta kuwa maisha yao yamebadilika ghafla.

MASWALI

a) Taja changamoto **nne** zinazowakumba wasichana waliojifungua. (alama 4)

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………..

b) “Kuvunjika kwa mwiko si mwisho wa upishi.” Eleza **ukweli** wa **kauli** hii kwa kurejelea kifungu. (alama 2)

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

c) Bainisha hatua **tatu** za serikali ili kuhakikisha wasichana wameendeleza elimu. (alama 3)

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………….

d) Kipe kifungu ulichosoma **anwani** mwafaka. ( alama 1)

…………………………………………………………………………………………

e) Tambua maudhui **matatu** muhimu yanayojitokeza katika kifungu hiki. (alama 3)

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………..

f) Eleza **maana** ya **msamiati** ufuatao kama ulivyotumika katika kifungu. (alama 2)

i. aula
………………………………………………………………………………………

ii. hamasisho

………………………………………………………………………………………

**2. UFUPISHO** **ALAMA 15**

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

Ikitambua hitaji la kuwianisha mipango yake na Malengo ya Ustawi Endelevu katika muongo huu wa utekelezaji, Serikali ya Kaunti ya Mandera imeamua kuchukua hatua zifaazo kwa manufaa ya watu wake. Muhimu miongoni mwa malengo haya ni kuondoa umaskini, njaa na hatua ya hali ya hewa. Mwitikio wetu kwa SDG's zinazoungwa mkono na umoja wa mataifa, umekua kupitia kuwianisha Mpango wa Ustawishaji wa Kaunti na wa Serikali ya Kitaifa na manifesto ya Gavana.

Uwiano huu umekuza ushirikiano na mashirika kama vile; Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP), RACIDA, World Vision, na mengine, na kuchangia upanuzi wa ardhi ya kilimo cha unyunyuziaji maji na uzalishaji wa chakula chenye virutubisho vingi ndani ya nchi. Kaunti ya Mandera inategemea sana mto Daua unaovuka mpaka, unaotumiwa na Kenya, Ethiopia na Somalia kwa unyunyiziaji. Kaunti hii pia hutumia visima kwa usambazaji wa maji. Miradi sita mikuu ya unyunyiziaji kando ya mto Daua, ikiwa ni pamoja na Malkakana, Hareri, Aresa, Khalalio, Gadudia na Border-Point One, imechangia kwa kiasi kikubwa shughuli za kilimo.

Serikali ya Kaunti, kwa ushirikiano na washirika wa maendeleo, hutoa msaada wa nyenzo na kiufundi kwa wakulima. Mashamba mashuhuri kama vile Wayame na Tattane yamenufaika na usaidizi huu, na hivyo kuchangia kuongezeka kwa hamu ya kilimo miongoni mwa wakazi wa Mandera. Ujenzi wa kisima cha maji cha Kutulo-Malbe ya mita mia mbili elfu, umeongeza zaidi shughuli za kilimo kwa kutoa njia mbadala ya kujikimu kwa wakulima pamoja na uzalishaji wa mifugo. Ili kuboresha ukabilianaji na ustahimilivu wa mabadiliko ya

tabianchi, Serikali ya Kaunti inakuza vitalu vya miti na vyandarua, na kuhimiza uanzishwaji wa bustani za jikoni na upandaji miti asilia na mkulima mmoja mmoja.

Kaunti hiyo inakumbatia nishati safi, kwa kupitishwa kwa pampu ya maji ya jua katika miradi ya umwagiliaji na kwa wakulima wadogo. Mbinu hii endelevu ya Chakula ya WFP inalenga katika kuimarisha uwezo wa jamii wa kuzalisha chakula na kuunda vyanzo mbadala vya kujikimu kimaisha. Kwa kushirikiana na serikali ya kaunti, WFP imefanya miradi kama vile ujenzi wa visima vifupi na mabwawa ya shamba. Pia hutoa msaada wa kiufundi na kuwajengea uwezo wakulima. Kuanzishwa kwa mazao yenye virutubishi vingi kama viazi vitamu vya rangi ya chungwa kumeonekana kuwa na mafanikio katika kukabiliana na utapiamlo. Juhudi za kaunti katika miundo ya uvunaji na uhifadhi wa maji, ikiwa ni pamoja na mabwawa ya shamba, sufuria za maji na visima vifupi, zimesaidia kuondoa changamoto zinazoletwa na mvua zisizo za kutosha na zisizo za kuaminika. Mipango hii imeathiri vyema uzalishaji wa kilimo na kuboresha maisha ya watu wa Mandera.

Mageuzi ya mtindo wa maisha katika ukanda huu, yaliwawezesha wafugaji wengi kukumbatia kilimo cha kiwango kidogo mbali na kufaulisha upanuzi wa mashamba ya kuzalisha mazao. Kwa sasa, zaidi ya hekta elfu nne na mia sita zimetengwa kwa ajili ya kilimo cha unyunyiziaji. Wamegeuza ardhi kame kuwa mashamba yenye faida. Mashamba mengi kwa sasa yanapendeza kutokana mvuto wa mazao mbalimbali yanayonawiri sana, si mahindi, si mboga, si matunda, kilimo kimetia fora na kupiga jeki juhudi za kuhakikisha utoshelevu wa chakula na kuleta kipato kwa wenyeji.

Ili kufanikisha hatua hii muhimu ya kihistoria, Serikali ya Kaunti hii ilitenga kiasi kikubwa cha pesa kwenye bajeti yake ya kila mwaka kwa ustawishaji wa kilimo na ufufuzi wa sekta hii. Leo hii, sehemu kubwa ya ardhi ambayo hapo awali ilisitiri vichaka, huzalisha mazao ya chakula kwa lengo la kuyauza katika soko la nje, kwa hakika, zao la tikiti-maji kutoka Mandera linatamaniwa sana na bila shaka ndilo tamu zaidi katika bara hili!

**MASWALI**

a) Ni **hatua** zipi zilizochukuliwa na kaunti ya Mandera ili **kuondoa njaa** na **umaskini**. Maneno (70-75) (alama 6, 1 mtiririko)

**Matayarisho**

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………

*©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]*

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

**Nakala Safi**

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

b) Fupisha ujumbe wa **aya tatu za mwisho**. Maneno (100-105) (alama 9, 1 mtiririko)

**Matayarisho**

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

*©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]*

…………………………………………………………………………………………

…………...………………………………………………………………………………

**Nakala Safi**

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

## 3. MATUMIZI YA LUGHA — ALAMA 40

a) Andika neno lenye **sauti** zenye **sifa** zifuatazo:
kipasuo kwaruzo hafifu cha kaakaagumu, irabu ya wastani viringwa, kipasuo hafifu cha ufizi, irabu ya mbele wastani (alama 1)

…………………………………………………………………………………………

b) Onyesha **muundo** wa silabi katika neno.
itifaki (alama 1)

…………………………………………………………………………………………

c) Weka **shadda** kwenye neno lifuatalo ili kutoa **maana mbili** tofauti.
Mbuni (alama 2)

***©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]***

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

d) **Ainisha** sentensi zifuatazo **kidhamira**. (alama 2)
Wekeni hapo!

……………………………………………………………………………………………

Naomba mtayarishe mashamba kwa wakati.

…………………………………………………………………………………………..

e) Ainisha **mofimu** katika neno lifuatalo.
Aliyemamrisha (alama 3)

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

f) i. Fafanua maana ya **mzizi huru**. (alama 1)

……………………………………………………………………………………………

ii. Toa **mifano** miwili ya mizizi huru (alama 1)

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

g) Tunga sentensi moja kuonyesha **matumizi mawili** ya **kinyota**. (alama 2)

……………………………………………………………………………………………

h) Geuza sentensi ifuatayo iwe katika **wakati uliopita hali timilifu**.
Kitabu kipya chanunuliwa na baba. (alama 2)

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

i) **Kanusha** sentensi ifuatayo. (alama 2)
Kucheza kwake kumemfanya ajulikane.

…………………………………………………………………………………………..

j) Tambua **miundo miwili** katika **ngeli** ya **U-I** kwa kutoa mifano mwafaka. (alama 2)

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

k) Tunga sentensi yenye **nomino ya jamii** pamoja na **kivumishi kirejeshi**. (alama 2)

***©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]***

…………………………………………………………………………………………………

l) Nyambua kitenzi **lia** katika kauli ya **kutendesha**. (alama 1)

…………………………………………………………………………………………………

m) Andika sentensi ifuatayo katika **ukubwa wingi**.
Mgeni wa mama alituletea mkate (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………

n) Tambua na ueleze aina za **vihusishi** katika sentensi ifuatayo.
Alirudi nyumbani kabla ya wakati kwa sababu mwanawe alianguka ndani ya shimo la maji. (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

……………………………..…………………………………………………………………

o) Andika sentensi ifuatayo **upya** kwa kufuata maagizo kwenye mabano. (alama 2)
Msasi aliwinda wanyama wakubwa kwa mishale. (**anza kwa shamirisho kipozi**).

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

p) Tumia neno **maskini** kama: (alama 2)
i,Kihisishi

…………………………………………………………………………………………………

ii.Kielezi

………………………………………………………………………………………...

q) Tunga sentensi **moja** kutofautisha maana ya maneno yafuatayo.
Jabari
Jabali (alama 1)

……………………………………………………………………………….....................

r) Bainisha maana **mbili** zinazojitokeza katika sentensi ifuatayo.
Bitugi alimpigia simu. (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

***©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]***

s) Onyesha matumizi ya **kiambishi -ji-** katika sentensi ifuatayo.
Jitu lile lilijikata kwa jisu la mwindaji. (alama 2)

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

t) Ainisha **virai** katika sentensi ifuatayo.
Barua iliyoandika rais ilitumwa jana asubuhi. (alama 2)

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

u) Tunga **sentensi** yenye **muundo** ufuatao.
KN(W+ $\bar{s}$ ) + KT (T+N) (alama 2)

……………………………………………………………………………………………

v) Tawanya ni kwa kusanya, zama ni kwa ____________, na nyesha ni kwa ___________
(alama 1)

w) Geuza neno lililopigiwa mstari kuwa **nomino dhahania**.
Polisi waliwaua <u>wahuni</u> waliosumbua wanakijiji. (alama 1)

……………………………………………………………………………………………

**4. ISIMUJAMII** **ALAMA 10**

Mhusika I: Bei ya jioni. bei ya jioni. Vitu freshi kabisa. Karibu customer. Unataka nikuuzie nini?

Mhusika II: Sukuma na hoho nne.

Mhusika I: vyote ni shilling 50 kwa kilo.

Mhusika II: Nifungie kilo mbili yah oho na sukuma kilo nne.

Mhusika I: Asante sana

a) Tambua **sajili** inayorejelewa (alama 2)

*©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]*

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

b) Tambua **sifa tano** zinazojitokeza katika sajili hii. (alama 5)

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

c) “Papa yangu amefungueko retio anadaka kusikiliza madakazo ya chioni”

Toa sababu **tatu** ambazo zinawafanya watu kufanya makosa haya wanapozungumza. (alama 3)

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

***©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]***

JINA……………………………………………………………………………………………NAMABARI……………………

SHULE……………………………………………………………………………………TAREHE…………………………

DARASA…………………………………………………………………………………SAHIHI………………………………

**102/1**

**KISWAHILI**

**KARATASI YA 3**

**CLASS OF KCSE 2024**

**TIME: 2 ½ Hours**

# THE NYANZA & WESTERN REGIONS KCSE JOINT NATIONAL MOCK 2024

***Kenya Certificate of Secondary Education (KCSE)***

**MAAGIZO**

a) Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu
b) Jibu maswali manne pekee
c) Swali la kwanza ni la lazima
d) Maswali hayo mengine yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobakia yaani : Riwaya, hadithi fupi,ushairi na fasihi simulizi
e) Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja
f) Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili
g) Majibu yote sharti yaandikwe kwenye nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| USHAIRI | 20 | |
| TAMTHILIA | 20 | |
| RIWAYA | 20 | |
| HADITHI FUPI | 20 | |
| FASIHI SIMULIZI | 20 | |
| JUMLA | | |

*©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]*

**SEHEMU A:**

**FASIHI SIMULIZI**

**LAZIMA**

**1. Soma utungo ufuatao kasha ujibu maswali**

Mimi ni Olichilamgwara
Olichilamgwara mwana mbee wa Ojilong
Ojilong wa Marukatipe
Wazee waliposhindwa
Nilivuka misitu milima na mito
Ni mimi jabali
Kipande cha jifya la mama
Nilipokuwa nalisha mifugo
Nilisikia baragumu inalia
Baragumu ya wito
Mifugo wa mtemi wamechukuliwa
Nikachukua mkuki wangu
Wenye kigumba cha mti
Nikachukua upanga wangu
Wenye makali kama mmweso wa radi
Upanga uliopasua pembe za nyati kwa dhoruba moja
Ndipo nilipofyatuka kasi kama umeme
Kufumba kufumbua nikawakaribia nduli
Kusikia vishindi vyangu wakaanza kubabaika
Kuona kifua changu cha manyoya ya kanga wakatetemeka
Macho yangu makali kama kaa la moto yalipowatazama wakakimbia
Mkuki wangu ulipaa kama umeme
Wote wakalala
Mifugo wakanifuata…
Mko wapi vijana
Mmekuwa kama majivu baada ya moto kuzimika?

**Maswali**

a) Tambua kipera ulichokisoma na udhibitishe jibu lako (al. 2)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

b) Tambua sifa za jamii zinazosawiriwa katika utungo huu (al. 2)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

c) Kwa kutoa mifano bainisha vipengele vine vya kimtindo vilivyotumiwa na nafsineni (al. 4)

***©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]***

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

d) Fafanua sifa nne za kipera hiki (al. 4)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

e) Eleza mambo manne ambayo mtendaji wa kipera hiki anaweza kufanya ili kufanikisha utendaji wake. (al. 4)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

f) Fafanua mikakati ambayo jamii inaweza kutumia ili kuzuia tungo kama hizi kufifia (al. 4)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

**SEHEMU B:**

**TAMTHILIA: BEMBEA YA MAISHA, TIMOTHY AREGE**

**2. "Sima tayari. Ninaanda mchuzi….."**

a) Weka dondoo hili katika muktadha wake (al. 4)

b) Onyesha umuhimu wa msemewa wa maneno haya (al. 6)

c) Tambua toni katika dondoo hili (al. 2)

d) Eleza changamoto zinazokumba ndoa za kisasa kwa kurejelea tamthilia nzima (al. 8)

3. "Masombo hufungwa kama walau mtu ametia kitu mdomoni. Pamoja na hali ngumu iliyopo, bado hatujafikia pa kukosa mlo wa kimsingi. Ndiyo hatumudu viliwa vya samli lakini hatuwezi kuishi kama kwamba tunazongwa na njaa. Tazama ulivyokonda unaelekea kushindana na ng'onda. Hii nafasi ya ng'onda unaitaka kwa nini?

a) Weka dondoo hili katika muktadha wake (al. 4)

b) Tambua mbinu mbili za kimtindo zilizomo kwenye dondoo (al. 2)

c) Bainisha sifa nne za msemewa (al. 4)

d) Jadili namna msemaji amechangia katika kuendeleza

i) Ploti (al. 5)

ii) Maudhui (al. 5)

**SEHEMU C:**

**RIWAYA: Nguu Za Jadi la 4 au la 5**

4. Eleza umuhimu wa mandari ya ofisi ya chifu mshabaha ukirejelea riwaya ya nguu za jadi (al.20)

5. Jadili jinsi mwandishi wa riwaya ya nguu za jadi ameangazia dhana ya matumaini ( al 20)

**SEHEMU D:USHAIRI**

**USHAIRI**

**Jibu swali la 6 ay la 7**

**6. Soma shairi lifuatalo kasha ujibu maswali**

**Said A. Mohamed: Mbele ya Safari**

Ilipoanza safari, ilianza kwa dhiki
Tulishikana kwa ari, kwenda safari ya haki
Tukawa ni majabari, nyoyo zisitaharuki
Tukajizatiti

Njaa ikawa thabiti, na kiu kutamalaki
Nasi tulitia dhati, tusijali kuhiliki
Ingawa mbele mauti, dhila na mingi mikiki
Tulijizatiti.

Huu mwisho wa safari, tukaambiwa ni haki
Shangwe kwetu na fahari, utumwa hatuutaki
Kuwa mbele ya safari, juhudi iliyobaki
Tulijizatiti.

Ile ilikuwa ndoto, mwisho wake mafataki
Nguvu zimechomwa moto, sahala 'mmekuwa dhiki
Wagombania kipato, utashi haukatiki
Na kutabakari.

Msafara ukasita, kwenye mlima wa haki

*©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]*

Kijasho kinatuita, mlima haupandiki
Basi soe 'kajipeta, kukikwea kima hiki
Twataka hazina.

Tukiwa migongo wazi, tukainama kwa shaki
Tukawa'chia ukwezi, kialeni wadiriki
Wakapanda bila kazi, kuteremsha miliki
Wakaitapia.

Wakafikia makazi, ya pumbao na ashiki
Huko wakajibarizi, kwenye raha lakilaki
Wakaisahau ngazi, ya umma uliomiliki
Mbele ya safari.

Na hazina yetu sote, kuishusha hawataki
Wamo wanatema mate, kwa umati halaiki
Imezima nia yote, kiza hakitakasiki
Mbele ya safari.

**MASWALI**

a) Eleza safari inayorejelewa katika shairi hili (al. 2)

b) Onyesha kinaya cha safari inayozungumziwa (al. 3)

c) Taja na ueleze bahari mbili za shairi hili ukizingatia: (al. 2)

   i) Mizani

   ii) Vina

d) Andika ubeti wa saba kwa lugha ya nathari (al. 4)

e) Eleza umuhimu wa aina mbili za uhuru wa kishairi zilizotumiwa katika ubeti wa sita (al. 2)

f) Bainisha aina mbili za urudiaji zilizotumiwa katika shairi hili (al. 2)

g) Fafanua aina mbili za taswira zinazojitokeza katika shairi hili (al. 2)

h) Kando na kinaya, bainisha vipengele vingine viwili vya kimtindo katika shairi hili (al. 2)

i) Eleza toni ya shairi hili (al. 1)

**7. Soma shairi lifuatalo kasha ujibu maswali**

*©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]*

Ee mpwa wangu,
Kwetu hakuna muoga,
Uoga ukikufikia, huenda ni wa akina mamayo,
Fahali tilichinja ili uwe mwanamume,
Eewe mpwa wangu, kisu kikali ajabu!
Iwapo utatingisa kichwa,
Uhamie kwa wasiotahiri.

Wanaume wa mbari yetu,
Si waoga wa kisu,
Wao hukatwa kuanzia macheo hadi machweo,
Wewe ndiye wa kwanza,
Iwapo utashindwa,
Wasichana wote,
Watakucheka,
Ubaki msununu,
Simama jiwe liwe juu
Ndege zote ziangamie.

Simu nimeipokea,
Ngariba alilala jikoni,
Visu ametia makali,
Wewe ndiye wangojewa,
Hadharani utasimama,
Macho yote yawe kwako,
Iwapo haustahimili kisu,
Jiuzulu sasa mpwa wangu,
Hakika sasa mpwa wangu,
Hakika tutakusamehe, mwaka kesho unakuja.

Asubuhi ndio hiii,
Mama mtoto aamushwe,
Upweke ni uvundo,
Iwapo utatikisa kichwa.
Iwapo wewe ni mme,
Kabiliana na kisu kikali,
Hakika ni kikali!

Kweli ni kikali!
Wengi wasema ni kikali!
Fika huko uone ukali!
Mbuzi utapata,
Na hata shamba la mahindi,
Simama imara,
Usiende kwa wasiotahiri.

**Maswali**

a) Hili ni shairi la aina gani? Thibitisha (al. 2)

***©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]***

b) Tambua anayeimba na anayeimbiwa shairi hili (al. 2)

c) Toa ithibati kwenye shairi hili kuthibitisha kuwa msimulizi ana taasubi za kiume (al. 2)

d) Taja kwa kutolea mifano mbinu zozote nne za uandishi katika shairi hili (al. 4)

e) Taja shughuli zozote mbili za kiuchumi za jamii inayorejelewa katika shairi hili (al. 2)

f) Eleza mbinu alizotumia mshairi kutosheleza mahitaji ya kiuarudhi (al. 4)

g) Msamiati ufuatao umetumika kwa maana gani katika shairi hili? (al. 4)

i) Mbari

ii) Msununu

iii) Ngariba

iv) Uvundo

**SEHEMU E:**

**HADITHI FUPI**

**Harubu ya maisha *Paul Nganga Mutua***

"Naja. Nakamilisha shughuli ndogo hapa kisha nianze safari…"

(a) Weka dondoo hili katika muktadha wake (al. 4)

(b) Eleza sifa sita za msemaji wa kauli hii (al. 6)

(c) Jadili changamoto wanazokumbana nazo waajiriwa kwa kurejelea hadithi hii (al. 10)

…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………

*©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]*

©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]

*©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]*

*©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at*
*www.kenyaeducators.co.ke]*

*©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]*

©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]

**HUU NDIO UKURASA WA MWISHO KUPIGWA CHAPA!**

*©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]*

JINA.............................................................................................NAMABARI............................

SHULE...........................................................................................TAREHE.................................

DARASA......................................................................................SAHIHI.........................................

***102/1***
***KISWAHILI***
***KARATASI YA 1***
***CLASS OF KCSE 2024***
***Time: 2 ½ hours***

# THE COASTAL & EASTERN REGIONS KCSE JOINT NATIONAL MOCK 2024

***Kenya Certificate of Secondary Education (KCSE)***

**MAAGIZO KWA MTAHINIWA:**

1) Andika jina lako, nambari ya mtihani na tarehe katika karatasi ya majibu.
2) Karatasi hii ina maswali manne.
3) Jibu maswali mawili pekee. Kila swali lina alama ishirini.
4) Swali la kwanza ni la lazima.
5) Chagua swali jingine lolote kutoka kwa matatu yaliyosalia.
6) Majibu yote yaandikwe katika karatasi ya majibu uliyopewa.
7) Majibu yote yaandikwe katika lugha ya Kiswahili.

***Sehemu hii imehifadhiwa kwa matumizi ya mtahini pekee.***

| SWALI | 1 | 2 | 3 | 4 |
|---|---|---|---|---|
| UPEO | 20 | 20 | 20 | 20 |
| ALAMA | | | | |

**JUMLA**

| | |
|---|---|
| UPEO | 40 |
| ALAMA ZA MTAHINIWA | |

***©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]***

1. Lazima
   Andaamahojianokatiyamtangazajikatikaidhaayaya RedioMialenamtaalamuwa ushaurinasahakuhusuvyanzovyakuporomokakwamaadilimiongonimwavijana.

2. Tamashazamuziki, michezonashughulinyinginezonjeyadarasahuwapotezeawanafunziwakatiadimuwamasomonazafaakupigwamarufuku. Jadili.

3. Samakimkunjeangalimbichi

4. Andikainshaitakayochukuamwanzoufuatao.
   Ukumbiwamahakamaulikuwaumejaawatufurifuri. Mshtakiwaalikuwaameinamishausowake. Hatimayakesiiliyomkabiliilifahamikatunahakimu. Punde…

***©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]***

**JINA**.........................................................................................**NAMABARI**............................

**SHULE**.......................................................................................**TAREHE**.................................

**DARASA**...................................................................**SAHIHI**.........................................

***102/2***
***KISWAHILI***
***KARATASI YA 2***
***CLASS OF KCSE 2024***
***Time: 2 ½ hours***

# THE COASTAL & EASTERN REGIONS KCSE JOINT NATIONAL MOCK 2024

***Kenya Certificate of Secondary Education (KCSE)***

**Maagizo**

a) Andika jina lako na nambari yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
b) Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
c) Jibu maswali **yote**.
d) Majibu yote yaandikwe kwa nafasi ulizoachiwa.
e) Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya **Kiswahili**.

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| **Ufahamu** | **15** | |
| **Ufupisho** | **15** | |
| **Matumizi ya lugha** | **40** | |
| **Isimujamii** | **10** | |
| **JUMLA** | **80** | |

**1. UFAHAMU**

*©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]*

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

Takwimu ambazo zimetolewa na shirika la kazi la kimataifa (ILO) zinaonyesha kuwa ulanguzi wa watoto umetangaa hususan katika mataifa yanayoendelea. Ipo tumbi ya sababu za kuelezea kwa nini biashara hii imeshamiri.

Athari mojawapo ya utandawazi ni kuunda mtandao mpana ulimwenguni . Mtandao huo unaweza kutumiwa kwa njia chanya au njia hasi. Njia chanya ni zile zinazochukuliwa kuwafaidi wanajamii kwa kuendeleza ubinadamu na kuboresha hali ya maisha kiuchumi,kisiasa na kitamaduni. Maarifa yanayosambazwa kuwa chachu ya kuumua ari ya maendeleo,elimu na mafanikio katika mataifa mengi ulimwenguni. Njia hasi ni zile ambazo maarubu yake ni kuwanufaisha wachache huku zikiwahasiri wengi.

Kuwepo kwa mtandao kunawapa wenye nia tule kama usafirishaji na ulanguzi wa watoto fursa ya kuzitosheleza hawaa zao. Wanaoshiriki katika biashara huongozwa na pashau ya utajiri. Hawachelei kuwalangua watoto wanaochimbukia mataifa ya kimaskini huko ughaibuni wanakozongomezwa kwenye madanguro, kufanyishwa kazi za sulubu na za kitopasi na kuishi maisha duni .

Asilimia kubwa ya watoto hurubuniwa kwa ahadi ghushi za kujiendeleza kimasomo. Wengine huuzwa kutokana na msaada wa jamaa zao wanaotovukwa na utu na kuwa mawakala katika amali hii ya kusikitisha .Biashara hii huweza kusahilishwa kwa kuwepo kwa mfumo fisadi wa kisheria ,msambaratiko wa muundo wa jamaa na ubinafsi wa kijamii.

Ipo haja kubwa ya ushirikiano wa mataifa alkulihali kuikomesha biashara hii haramu. Jamii ya ulimwengu isipofanya hivi, itakuwa imekitia kizazi kizima kitanzi na kutumbukiza kesho yake kwenye matatizo kathiri.

a) Ni kwa jinsi gani utandawazi umechangia katika biashara ya ulanguzi wa watoto? (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

b) Mwandishi wa kifungu anapendekeza hatua zipi kusuluhisha tatizo la ulanguzi wa watoto? (alama 3)

***©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]***

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

c) Eleza jinsi watoto wanaolanguliwa wanavyoishi huko ughaibuni. (alama 3)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

d) Kulingana na muktadha, kifungu " chachu ya kuumua ari ya maendeleo" kina maana gani ? (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

e) Jamii isiyosuluhisha tatizo la ulanguzi wa watoto itakuwa na hatima gani ? (alama3)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

f) Eleza maana ya (alama 2)

i. Maarubu…………………………………………………………………………

ii. Pashau…………………………………………………………………………

2. **UFUPISHO**(Alama15)

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Tangu enzi ya ukoloni mkongwe, Wakenya wamekuwa wakipigania ukombozi wao. Awamu ya kwanza ya ukombozi ilipatikana miaka ya sitini, hasa mwaka wa 1963 tulipojinyakulia uhuru wa kujitawala kutoka kwenye utawala wa Mwingereza. Ukombozi huu uliwezesha Wakenya asilia

kushikilia awamu za uongozi. Ili kuwezesha Wakenya kujitawala, walikabidhiwa katiba mpya iliyotayarishwa na Mwingereza. Hata hivyo, wazalendo halisi hawakutosheka na katiba hii. Kutokana na hali hii, harakati za kujipatia ukombozi wa pili zilianza mara tu baada ya kupatikana kwa ukombozi wa kwanza. Ni kweli kuwa badiliko kwa mjukuu huanza kwa babu. Wazalendo wa zama hizo wakaanza kupigania kubadilisha na kurekebishwa kwa katiba, na hapa ndipo mbegu ya kutafuta mabadiliko ilipopandwa. Harakati hizi ziliendelea hadi mwaka 2010 wakati Wakenya walipopitisha katiba mpya inayotumiwa hivi sasa kuongoza nchi hii. Katiba hii inatarajiwa kuleta ugatuzi katika uongozi wa nchi. 'Ugatuzi' maana yake ni kuhamisha mamlaka kutoka kwenye viongozi wa ngazi za juu na kuyakabidhi raia wenyewe. Ni sawa na kupewa shamba ambalo bado halijalimwa ili wenyewe walifyeke, walime, wapande, wapalilie na wavune. Ijapo njia hii ya kujitawala ni ngeni na yenye changamoto nyingi, wengi wa Wakenya wanaifurahia.

Je, unafikiria Wakenya wameichangamkia katiba hii eti kwa sababu tu ni mpya? Itategemea uamuzi na umakinifu wa kila mmoja wetu na matumaini aliyo nayo kutokana na katiba yenyewe. Mimi ninapoichunguza na kuitalii katiba hii sikubaliani na methali eti *kipya kinyemi ingawa kidonda*. Ni kweli kuwa macho mengi huona kuliko jicho moja. Katiba hii ni nzuri kwa kuwa inashirikisha watu wengi katika kupanga na kutekeleza miradi ya maendeleo. Kutokana na juhudi hii, asilimia kubwa ya wananchi hushirikishwa katika kufanya uamuzi wa masuala yanayowahusu maishani mwao. Talanta mbalimbali zinaweza kuimarishwa ili ziweze kutumika vilivyo na kuchangia juhudi za maendeleo.

Isitoshe, katiba hii ni nzuri kwa vile inachangia kupeleka mamlaka na ugawaji wa rasilimali mashinani mwa nchi. Jambo hili litasaidia sana kuleta mamlaka na maendeleo karibu na raia ili waweze kuishi maisha bora kuliko hapo awali. Ukichunguza nchi hii, ni dhahiri kuwa kuna sehemu ambazo zimepiga hatua kubwa kimaendeleo kuliko zingine. Ili kustawisha maendeleo katika pembe zote za nchi, mfumo wa ugatuzi utagawa fedha za makadirio ya matumizi kwa kuzingatia viwango vya umaskini katika kila kaunti. Hali hii itawezesha kaunti zote nchini kujimudu na hivyo kuinua kiwango cha maendeleo katika nchi nzima.

Mfumo huu wa utawala hubidi washika dau kuketi pamoja na kupanga mipango kabambe inayohusu maendeleo ya kaunti ama sehemu husika. Jambo hili huwapa nafasi wahusika kutambua mahitaji ya kimsingi ya maeneo yao ili yaweze kupewa kipaumbele katika utekelezaji, na hivyo wanaoshirikishwa katika utekelezaji wa mradi husika huiunga mkono kikamilifu na hivyo kuleta hali ya uelewano na utangamano. Uelewano huu huwezesha maendeleo kupatikana kwa haraka ukilinganisha na hali ambapo mipango hii ingepangwa na kutekelezwa na watu kutoka nje wasioelewa matakwa ya wakazi wa sehemu husika.

***©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]***

Katiba hii pia inasaidia kueneza na kutilia mbolea mfumo wa kidemokrasia katika nyanja zote za maisha. Katika miaka ya hivi karibuni kumetokea mabadiliko ulimwenguni kote na watu wengi wanatarajia demokrasia itawale katika maamuzi ya shughuli zote za maisha yao. Wananchi hujiona kuwa wenye umuhimu mkubwa kwa vile wao wenyewe ndio hujitawala na haki zao hutiliwa maanani. Wana uhuru wa kusema, kuabudu, kutoa maoni, kushiriki, kusisitiza utawala wa kisheria na wa walio wengi, pamoja na haki za wachache kuheshimiwa. Hata hivyo, haimaanishi kuwa anapopewa uhuru huu mtu ana kibali cha kukandamiza wenzake kwa kutozingatia sheria.

Katiba hii ya ukombozi wa pili wa Kenya imewapa wananchi msukumo na matumaini makuu kuwa milango ya heri itafunguliwa bila kujali umri, jinsia, tabaka, kabila, asili au hata mbari za wananchi.

a) Kwa kurejelea aya ya kwanza, onyesha jinsi wazalendo hawakutosheka na katiba ya kwanza ya Kenya. (Maneno 40- Alama 5, 1 mtiririko)

**Matayarisho**

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

**Nakala safi**

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

***©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]***

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

b) Eleza kwa nini Wakenya wameichangamkia katiba mpya.(Maneno 60- Alama 10, 2 mtiririko)

**Matayarisho**

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

**Nakala safi**

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

*©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]*

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

3)**MATUMIZI YA LUGHA** (Alama 40)

a) Andika **sauti** yenye sifa zifuatazo: (Alama1)

i. Konsonanti
ii. hutamkiwa kaakaa laini
iii. kikwamizo ghuna

……………………………………………………………………………………………………

b)Tofautisha maana ya sentensi zifuatazo: (Alama2)

i) Kazi yote ni muhimu.

……………………………………………………………………………………………………

ii) Kazi yoyote ni muhimu.

……………………………………………………………………………………………………

*©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]*

c) Andika sentensi ifuatayo katika wakati uliopita , hali isiyodhihirika. (Alama2)

Kenya hupokea watalii wengi.

…………………………………………………………………………………………………

d)Tunga sentensi ukitumia **ni**kama: (Alama 3)

i)kitenzi

…………………………………………………………………………………………………

ii)kiwakilishi

…………………………………………………………………………………………………

iii)kielezi

…………………………………………………………………………………………………

e)**Yakinisha** sentensi hii : (Alama2)

Haji kukuona wala hataenda kesho.

…………………………………………………………………………………………………

f) i) **Silabi** ni nini? (Alama2)

…………………………………………………………………………………………………

ii) Huku ukitoa mifano , eleza aina mbili za silabi za Kiswahili. (Alama2)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

g) Ainisha **virai** katika sentensi: (Alama2)

Jirani mwenye lile shamba kubwa husaidia maskini.

…………………………………………………………………………………………………

***©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]***

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

h) Huku ukitoa mifano mwafaka onyesha matumizi mawili ya **kinyota (*)** katika sarufi ya Kiswahili. (Alama4)

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

i) Andika sentensi hii kwa **usemi halisi:** **(**Alama 2)

Jane alimwamuru yaya wake aache uzembe kazini.

…………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

j) Neno **unga** lina maana ya nafaka iliyosagwa. Eleza maana nyingine mbili. (Alama 2)

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

k) Andika **ukubwa**wa: (Alama2)

Mwanamke mpiga ngoma aliiba mtoto na kumtia kwenye kikapu.

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

l) Tunga sentensi mojamoja kuonyesha matumiziya vitenzi hivi katika hali ya **kutendesha** . (Alama 2)

i)nywa

……………………………………………………………………………………………………

***©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]***

ii)fa

…………………………………………………………………………………………………

m) Changanua kwa njia ya **mishale** : (Alama 4)

Wezi waliotaka kuiba walifukuzwa na bawabu.

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

n) Unda **sentensi moja** yenye sehemu zifuatazo: (Alama 2)

i)kikanushi cha nafsi ya kwanza umoja.

ii)wakati ujao

iii)yambwa tendwa

iv)mzizi

v)kauli ya kutendesha

vi)kiishio

…………………………………………………………………………………………………

o)Jaza mapengo kwa**kinyume** cha neno lililopigiwa mstari: (Alama 1)

Kuchomozakwa jua kulimpa matumaini ambayo yalififishwa nakwake.

p) Eleza matumizi ya **kwa**katika sentensi: (Alama 2)

Kwa nini alipata moja kwa tano ilhali angesaidiwa na mwalimu kwa sababu kwa mwalimu si mbali.

***©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]***

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

q) Tunga sentensi mbili kuonyesha matumizi mawili tofauti ya kiwakilishi**‘li’**. (Alama 2)

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

r) Toa maana ya **nahau** : (Alama 1)

kushika miguu

……………………………………………………………………………………………………

***©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]***

**4. ISIMUJAMII**(Alama 10)

a)Fafanua sifa zozote sita za sajili ya**shuleni** . (Alama 6)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

b)Eleza jinsi **malezi** yanavyodhibiti mitindo ya lugha. (Alama 4)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

**HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA**

***©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]***

**JINA...............................................................................................................NAMABARI...........**

**SHULE...........................................................................................................TAREHE.................**

**DARASA.....................................................................................................SAHIHI.......................**

***102/3***
***KISWAHILI***
***KARATASI YA 3***
***CLASS OF KCSE 2024***
***Time: 2 ½ hours***

# THE COASTAL & EASTERN REGIONS KCSE JOINT NATIONAL MOCK 2024

***Kenya Certificate of Secondary Education (KCSE)***

**MAAGIZO**

a) Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu
b) Jibu maswali manne pekee
c) Swali la kwanza ni la lazima
d) Maswali hayo mengine yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobakia yaani : Riwaya, hadithi fupi,ushairi na fasihi simulizi
e) Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja
f) Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili
g) Majibu yote sharti yaandikwe kwenye nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| USHAIRI | 20 | |
| TAMTHILIA | 20 | |
| RIWAYA | 20 | |
| HADITHI FUPI | 20 | |
| FASIHI SIMULIZI | 20 | |
| JUMLA | | |

**SEHEMU A: USHAIRI (ALAMA 20)**

**1. LAZIMA**

Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

Alikwamba wako mama, kajifanya hupuliki,
Kakuasa kila jema, ukawa ng'oo!Hutaki,
Sasa yamekusakama, popote hapashikiki,
Uliyataka mwenyewe!

Babayo lipokuonya, ukamwona ana chuki,
Mambo ukaboronganya, kujifanya hushindiki,
Sasa yamekunganya, kwa yeyote hupendeki,
Uliyataka mwenyewe!

Mazuri uliodhania, yamekuletea dhiki,
Mishikeli miania, kwako ona haitoki,
Mwanzo ungekumbukia, ngekuwa huaziriki,
Uliyataka mwenyewe!

Dunia nayo hadaa, kwa fukara na maliki,
Ulimwenguni shujaa, hilo kama hukumbuki,
Ya nini kuyashangaa? Elewa hayafutiki,
Uliyataka mwenyewe!

Mwenyewe umelichimba, la kukuzika handaki,
Ulijidhania samba, hutishiki na fataki,
Machungu yamekukumba, hata neno hutamki,

***©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]***

Uliyataka mwenyewe!

Kwa mno ulijivuna, kwa mambo ukadiliki,

Na tena ukajiona, kuwa wewe mstahiki,

Ndugu umepatikana, mikanganyo huepuki,

Uliyataka mwenyewe!

**Maswali**

1.Shairi hili ni la **aina** gani? Eleza (alama 2)

2.Ukizingatia vigezo vifuatavyo,taja **aina za bahari** za shairi (alama 3)

i. Kibwagizo

ii. Vina

iii. Vipande

3.Tambua kwa kutoa mifano **mitatu** ya mbinu ambazo mshairi ametumia ili kutosheleza mahitaji ya kiarudhi**.** (alama 3)

4.Eleza **muundo** wa ubeti wa **tano.** (alama 4)

5.Taja na utoe mifano ya aina zozote **mbili za tamathali za usemi** zilizotumika katika shairi. (alama 2)

6.Bainisha **toni** ya shairi hili. (alama 2)

7.Andika ubeti wa **pili** kwa **lugha ya nathari**. (alama 4)

**SEHEMU B:TAMTHILIA**

**Timothy M.Arege :Bembea ya Maisha**

**Jibu swali swali la 2 au la 3**

*©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]*

2. “Maisha ya sasa hayana fundi.Yanamwendesha kila mtu kama tawi lililosukumwa hadi likang’oka kutoka taagani na kupeperushwa na upepo…Ulimwengu wa sasa haubagui. Wadogo kwa wakubwa”.

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

b) Huku ukitoa mifano, changanua **mbinu tano za uandishi** ambazo zimejitokeza katika nukuu. (alama 10)

c) Kukatika kwa bembea haiwi mwisho wa mchezo huunganishwa na mchezo kuendelea.

Kwa kutoa mifano **sita** onyesha jinsi wahusika mbalimbali **walivyounganisha** bembea yao ya maisha. (alama 6)

3. Mabadiliko katika maisha ya mwanadamu hayana budi kumfika.Wakati mwingine mabadiliko haya huleta heri au mahangaiko. Jadili kwa kutoa mifano **jinsi wahusika mbalimbali walivyokumbwa na mabadiliko haya** ukirejelea tamthilia ya ‘Bembea ya Maisha’. (alama 20)

**SEHEMU C: RIWAYA**

**Clara Momanyi: Nguu za Jadi**

**Jibu swali la 4 au 5**

4. “Tangu lini mke amuulize mumewe kule aendako au atokako?.....Ama kweli, wanawake wa kisasa wanavunja kila mwiko uliowekwa na wazee.”

i) Yaweke maneno haya katika **muktadha** wake. (alama4)

ii) Kwa kutoa mfano,**taja mbinu ya lugha** iliyotumika. (alama2)

iii) Eleza **umuhimu wa msemaji** (alama4)

*©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]*

(iv) Kwa kutoa mifano **kumi** kutoka riwayani, fafanua jinsi **mwanamke amesawiriwa** katika jamii ya Matuo. (alama 10)

5. Jamii ya Matuo katika riwaya ya 'Nguu za Jadi' imekumbwa na **usaliti** si haba. Kwa kutoa mifano mwafaka riwayani, onyesha ukweli wa kauli hii. (alama20)

**SEHEMU D: HADITHI FUPI**

**MAPAMBAZUKO YA MACHWEO NA HADITHI NYINGINE**

**Jibu swali la 6 au 7**

**'Mapambazuko ya Machweo'**

6. "Una pesa ya kulipa teksi?"

a) Eleza **muktadha** wa dondoo hili. (alama 4)

b) Taja **mbinu mbili za lugha** ambazo zimejitokeza katika dondoo hili kwa kutoa mifano. (alama2)

c) Kwa kutolea hoja **nne**, onyesha **umuhimu wa mnenewa** katika kukuza vitushi vya hadithi hii. (alama 4)

d) Eleza jinsi anwani 'Mapambazuko ya Machweo' **ilivyoafiki hadithi** hii kwa kutoa mifano **kumi** kutoka hadithini . (alama 10)

"**Fadhila za Punda**"

7. "Yu wapi kirukanjia wako? Wajua yuko wapi? Uliacha mbachao kwa msala upitao. Atakutunza nani, maana kwako fadhila za punda ni mashuzi!"

a) Yaweke maneno haya katika **muktadha** wake. (alama 4)
b) Tambua **tamathali mbili za usemi** zilizotumika katika dondoo hili. (alama 2)
c) Fafanua **sifa zozote nne za anayeambiwa** maneno haya. (alama 4)

*©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]*

d) Kwa kurejelea hadithi 'Fadhila za Punda' onyesha **jinsi wanawake wanadhulumiwa** na jinsia ya kiume kwa kutoa **mifano kumi** mwafaka kutoka hadithini. (alama10)

**SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI**

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

8. Hapo zamani za kale paliishi sungura na ndovu.Wanyama hawa waliishi baharini. Mauluna alikuwa amewatunukia mapenzi si haba. Makazi yao yalikuwa yamepambwa yakapambika. Walitegemea matunda mbalimbali yaliyokuwa baharini kama mapera, matomoko, matikitimaji na kadhalika.

Siku moja usiku wa manane, maji yakaanza kupwa. Ndovu aliathirika zaidi. Alijaribu kuinama majini lakini hakuweza. Alimwita sungura amsaidie lakini sungura alikuwa ametoweka.

Ndovu aliamua kwenda kumtafuta sungura. Alimtafuta hadi msituni lakini hakumpata. Alihofia kurudi baharini na hadi wa leo yumo msituni.

**Maswali**

a)Tambua **utanzu** huu na **kipera** chake. (alama2)

b)Eleza **sifa tano za utanzu** wa kipera hiki. (alama3)

c)Eleza **umuhimu wa fomyula ya kuhitimisha** katika aina hii ya ngano. (alama 3)

d)Wewe ni fanani anayewasilisha kipera hiki kwa hadhira.Taja mambo **matatu** ambayo utafanya kuhakikisha **umefanikiwa katika uwasilishaji** wako. (alama 3)

e)Taja **manufaa mawili** ya ngano katika jamii. (alama 2)

f)Kipera hiki **kinaendelea kudidimia** katika jamii yako.Eleza **mbinu tano utakazozitumia kukidumisha** katika jamii ya leo. (alama5)

*©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]*

**JINA.............................................................................................NAMABARI............................**

**SHULE.........................................................................................TAREHE..................................**

**DARASA..........................................................................SAHIHI.........................................**

**102/1**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 1**
**CLASS OF KCSE 2024**
**TIME: 2 ½ HOURS**

# THE RIFT VALLEY & NORTH EASTERN KCSE JOINT NATIONAL MOCK 2024

Kenya Certificate of Secondary Education (KCSE)

**MAAGIZO KWA MTAHINIWA:**

1) Andika jina lako, nambari ya mtihani na tarehe katika karatasi ya majibu.
2) Karatasi hii ina maswali manne.
3) Jibu maswali mawili pekee. Kila swali lina alama ishirini.
4) Swali la kwanza ni la lazima.
5) Chagua swali jingine lolote kutoka kwa matatu yaliyosalia.
6) Majibu yote yaandikwe katika karatasi ya majibu uliyopewa.
7) Majibu yote yaandikwe katika lugha ya Kiswahili.

***Sehemu hii imehifadhiwa kwa matumizi ya mtahini pekee.***

| **SWALI** | **1** | **2** | **3** | **4** |
|---|---|---|---|---|
| **UPEO** | **20** | **20** | **20** | **20** |
| **ALAMA** | | | | |

**JUMLA**

| | |
|---|---|
| **UPEO** | **40** |
| **ALAMA ZA MTAHINIWA** | |

***©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]***

**1. Lazima.**
Umepata tangazo la nafasi ya kazi ya uhariri katika shirika la uchapishaji wa vitabu vya fasihi andishi kwenye gazeti la Taifa Leo. Andika barua ya kuomba nafasi hii na uambatanishe na wasifu kazi wako kwa maelezo zaidi.
**(Alama 20)**

**2.** Utelekezaji wa mtoto wa kiume nchini ni janga kuu. Jadili. **(Alama 20)**

**3.** Andika insha inayoafikiana na methali Baniani mbaya kiatu chake dawa.

**(Alama 20)**

**4.** Andika insha itakayomalizikia kwa;
…walipofungua mlango huo hatimaye,wengi hawakuweza kuzuia hisia zao.Waliangua vilio kwa maafa waliyoyashuhudia. **(Alama 20)**

*©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]*

**JINA.................................................................................................NAMABARI..............................**

**SHULE..............................................................................................TAREHE...................................**

**DARASA.......................................................................................SAHIHI..........................................**

**102/2**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 2**
**CLASS OF KCSE 2024**
**TIME: 2 ½ HOURS**

# THE RIFT VALLEY & NORTH EASTERN KCSE JOINT NATIONAL MOCK 2024

Kenya Certificate of Secondary Education (KCSE)

**Maagizo**

a) Andika jina lako na nambari yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
b) Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
c) Jibu maswali **yote**.
d) Majibu yote yaandikwe kwa nafasi ulizoachiwa.
e) Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya **Kiswahili**.

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| **Ufahamu** | **15** | |
| **Ufupisho** | **15** | |
| **Matumizi ya lugha** | **40** | |
| **Isimujamii** | **10** | |
| **JUMLA** | **80** | |

## 1 UFAHAMU (alama 15)

*©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]*

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali*

Suala la mahusiano ya wanadamu katika jamii, uainishaji wake na udhihirikaji wake limewashughulisha wataalamu wa elimu jamii kwa dahari ya miaka. Suala hili huwatafakarisha wataalamu hao kutokana na umuhimu wake katika maisha ya binadamu. Msingi mkuu wa uainishanji wa mahusiano hayo ni kukichuza kipindi cha mahusiano yenyewe. Yapo mahusiano bainaya waja ambayo yanachukua muda mfupi, kwa mfano saa au dakika chache na mengine ambayo huenda yakachukua miaka ayami.

Mahusiano ya muda mrefu kabisa ni yale yanayojulikana kama mahusiano ya kudumu. Inamkinika kudai kuwa miundo ya kijamii, kisiasa na kiuchumi huweza kuyadhibiti mahusiano hayo kwa kiasi kikubwa. Watu wengi huitakidi kuwa uhusiano uliopo baina ya mtu na jamaa yake utachukua muda mrefu, na kwa hiyo ni uhusiano wa kudumu. Hali hii hutokana na uhalisi kuwa tunahusiana na jamaa zetu kwa kipindi kirefu labda tangu ukembe hadi utu uzima wetu. Uhusiano huuhautarajiwi kuvunjwa na umbali wa masafa baina yetu;tunaendelea kuwasiliana kwa barua au, katika enzi hii ya utandawazi,kwa kutumia nyenzo za teknohama kama mtandao na simu za mkononi na kudumisha uhusiano wetuwa kijamaa. Hata hivyo, inawezekana baadhi ya mahusiano ya kijamaa yasiwe ya kudumu. Mathalan, uhusiano uliopo baina ya mke na mume, na ambao unatarajiwa kuwa wa kudumu au wa kipindi kirefu,unaweza kuvunjwa kwa kutokea kwa talaka. Talaka hiyo inavunja ule uwezekano wa uhusiano wa kudumu unaofumbatwa na sitiari ya pingu za maisha.

Katika ngazi ya pili,mahusiano ya kipindi cha wastani,kuna mahusiano yanayohusisha marafiki zetu maishani, shuleni au kwenye taasisi zozote zile, majirani zetu, wenzetu katika mahali mwa kazi,washiriki kwenye sehemu za ibada au za burudani na wenzetu kwenye vyama tofauti na makundi ya kujitolea. Inawezekanakudahili kuwa baadhi ya mahusiano haya,hususan baina ya marafiki na majirani huweza kuwa ya miongo na daima. Hali hii huweza kutegemea muundo na mfumo wa jamii. Kwa mfano, kwa wanajamii waoishi kwenye janibu fulani mahsusi, na kwa miaka tawili bila ya kuhajiri,uhusiano wao na majirani huweza kuwa wa kudumu. Hali hii **inasigana** na hali iliyoko kwenye maisha ya mijini. Maisha ya mijini yana sifa ya kubadilikabadilika. Isitoshe,kutokana na mfumo wa maisha ya kibepari **yameghoshi** ubinafsi mwingi. Mawimbi ya mabadiliko na ubinafsi huweza kuumomonyoaukuta wauhusiano wa kudumu.

Mwelekeo wa maisha ya siku hizi ya uhamaji kutoka maeneo au viambo walikoishi watu unasababisha kupombojea kwa mahusiano ya kudumu baina yao na majirani zao. Uhusiano katiya wenza katika mazingira ya kazi unahusiana kwa kiasi fulani na ule wamajirani. Vimbunga

**©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]**

vya ufutwaji kazi, ubadilishaji wa kazi, hali zisizotegemewa na mifumo ya kimataifa pamoja na hata mifumo ya kisiasahuweza kuathiri mshikamano wa wanaohusika kazini.

Kiwango cha mwisho cha mahusiano ni uhusiano wa mpito au wa muda mfupi. Mahusiano ya aina hii hujirikatika muktadha ambapo pana huduma fulani. Huduma hizi zinaweza kuwa za dukani, kwenye sehemu za ibada,kwenye kituo cha mafuta,kwa kinyozi, kwa msusi na kadhalika. Kuna sababu kadha zinazotufanya kuyazungumzia mahusiano ya aina hii kama ya mpito. Kwanza, uwezekanowa mabadiliko ya anayeitoa huduma hiyo ni mkubwa. Si ajabu kuwa unaporudi kwa kinyozi au msusi unatambua aliyekushughulikia hayupo. Hata hivyo, kuna **vighairi** hususa pale ambapo mtoa huduma anayehusika ni yule yule mmoja.

Mahusiano ya mpito yanatawaliwa na'uhusiano wa chembe chembe.' Uhusiano wa chembe chembe, bidhaa ya mfumo wa kibepari, unamaanisha kuwa kinachoshughulisha mtu ni chembe ndogo tu ya mwenzake. Chembe hiyo inaweza kuwa huduma, kwa mfano, gazeti analokuuzia mtu, viatu anavyokushonea,nguo anazokufulia,ususi anokufanyia na kadhalika. Mahussiano ya aina hii yametovukwa na hisia za utu na ni zao la mifumo ya kisasa ya kiuchumi na kijamii. Mtu anayehusiana na mwenzakekwa misingi ya chembe ndogo tu, huenda asijali kama mwenzake amekosa chakula,amefutwa kazi,amefiliwa,ameibiwa na kadhalika.
Suala kuu tunalopaswa kujiuliza ni: je, tunahusianavipi na jamaa zetu, marafiki zetuna majirani zetu? Je, uhusianowetu na raia wenzetu ni wa aina gani? Je, uhusiano wetu na nchi yetu ni wa mpito au ni wa kudumu?

(a) Taja kigezo cha kuzungumzia mahusiano. (alama 1)

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

(b) Eleza imani ya watu kuhusu mahusiano ya watu. (alama 1)

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

(c) Fafanua athari ya teknolojia kwenye mahusiano ya watu. (alama 2)

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

***©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]***

…………………………………………………………………………………………………………………………

(d) Eleza sababu nne kuu za kuharibika kwa mahusiano katika maisha ya leo.(alama 2)

…………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

(e) Taja sifa kuu za mahusiano ya muda mfupi. (alama2)

…………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

(f) Je, kifungu hiki kina ujumbe gani mkuu? (alama2)

…………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

(g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika kifungu. (alama 3)

(h) (i) inasigana…………………………………………………………………………………………………

(ii)yameghoshi…………………………………………………………………………………………………

(iii)vighairi……………………………………………………………………………………………………

## 2 UFUPISHO (alama 15)

Jamii ya leo inatawaliwa na kuendeshwa na kanuni ya maarifa. Inawezekana kusema kuwauchumi wa jamii za leo na zijazo utategemea maarifa zaidi kuliko utakavyotegemea uwezo wowote mwingine. Utambuzi wa uwezo mkubwa wa maarifa katika maisha ya binadamu ndio msingi wa watu kusema 'maarifa ni nguvu.'

Maarifa huelezwa kwa tamathali hii kutokana na uwezo wa: kuyadhibiti,kuyaendesha, kuyatawalana kuyaongoza maisha ya binadamu popote pale walipo. Mtu ameyakosa maarifa fulani huwa ameikosa nguvu hiyo muhimu na maisha yake huathirika pakubwa. Kwa msingi huu, maarifa yanawezakuangaliwa kama utajiri mkubwa ambao binadamu anaweza kuutumia kwa faida yake au kwa faida ya wanajamii wenzake. Ukweli huu ndio unaoelezwa na methali ya Kiswahili: 'Elimu ni mali.' Elimu ni chimbuko la maarifa muhimu maishani.

Msingi wa utajiri na maendeleo ya binadamu popote alipo basi ni maarifa. Je, maarifa kwa upande wake yana sifa gani? Maarifa yenyewe hayana upinzani. Maarifa uliyo nayo huweza kuwa na watu wengine pasiwe na upinzani baina yenu kwa kuwa kila mmoja ana maarifa sawa. Kila mmoja ana uhuru wa kuyatumia maarifa hayo kama chanzo cha kuyazalisha mengine. Utumiaji wa maarifa yenyewe hauyamalizi maarifa hayo. Maarifa hayawezi kugusika ingawa mtu anaweza kuyanyumbua maarifa yenyewe kwa kuyatumia kwa namna tofauti.

Maarifa huingiliana na maarifa mengine. Maarifa aliyo nayo mtu huweza kuhusishwa na maarifa aliyo nayo mtu mwingine ili kuvyaza au kuzuka na maarifa tofauti. Maarifa yanaweza kuchukuliwa kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa namna ambavyo mtu huweza kufanya bidhaa nyingine ile. Kwa mfano, ni muhali mtu kulalamika kuwa hawezi kutembea kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa sababu ana mzigo wa maarifa kichwani.

Sifa nyingine muhimu ya maarifa ni kuwa yanaweza kuwasilishwa kwa njia au mitindo mingine ya kidhahania. Ikiwa unataka kukihamisha chombo fulani kutoka sehemu moja hadi nyingine, lazima uwazie ukubwa wake, uzito wake na labda hata umbali wa panapohusika. Maarifa huweza kubadilishwa au kugeuzwa na kuwa ishara

***©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]***

ambazo huyafanya kuwasilishswa kwa njia nyepesi kuliko kwa mfano ikiwa mtu atayawasilisha katika muundo wa, kwa mfano,kitabu.

Maarifa yana sifa ya uhusianaji. Kipengele fulani cha maarifa huwa na maana kinapowekwa sambabmba au kugotanishwa na kipengele kingine cha maarifa. Huo huwa muktadha mzuri wa kueleweka au kuwa na maana kwa mfano, neno 'mwerevu' huweza kuwa na maana kwa kuwekwa katika muktadha wa 'mjinga', ' mjanja', 'hodari' na kadhalika.

Maarifa huweza kunifadhiwa katika nafasi ndogo sana. Suala hili linaeleweka kwa njia nyepesi tunapoangalia maarifa katika muktadha wa teknolojia. Data zinazowahusu mamilioni ya watu,ambazo zingehitaji maelfu ya maktaba na lukuki ya vitabu, huweza kuhifadhiwa kwenye kifaa kidogo kinachoweza kutiwa mfukoni.

Maarifa hayawezi kuthibitiwa au kuzuiliwa mahali fulani yasisambae. Maarifa huenea haraka sana. Maarifa ni kitu kinachoepuka pingu za watu wanaopenda kuwadhibiti binadamu wenzao. Hata pale ambapomfumo wa kijamii au wa kisiasa unafanya juu chini kuwadhibiti raia au watu wenyewe,ni muhali kuyadhibiti maarifa yenyewe. Inawezekana kuzidhibiti njia fulani za uenezaji wa maarifa lakini maarifa hayo yatapata upenyu wa kusambaa. Ni kweli kuwa maarifa ni nguvu inayozishinda nguvu zote.

(a ) Fupisha aya ya pilina tatu (maneno 55-60)(alama 5, 1 ya utiririko)

**Matayarisho**

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

*©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]*

……………………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………

**Nakala safi**

……………………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………

(b) Eleza sifa kuu za maarifa kama zinavyojitokeza kuanzia aya ya nne hadi aya ya nane.
(maneno 100-110) (alama 10, 2 za utiririko)

**Matayarisho**

……………………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………

*©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]*

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

**Nakala safi**

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

*©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]*

…………………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………………

**3 MATUMIZI YA LUGHA** (alama 40)

(a) Taja vipasuo sighuna (alama 2)

……………………………………………………………………………………………………………

(b) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao:
kirai nomino, kirai tenzi, kirai husishi (alama 2)

……………………………………………………………………………………………………………

(c ) Bainisha shamirisho na chagizo katika sentensi (alama 2)

Vibarua wamefanya kazi haraka ipasavyo .

……………………………………………………………………………………………………………

(d) Sahihisha

Mwalimu mwenye alikuja jusi anafudisha Kiswahili vizuli. (alama 2 )

*©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]*

……………………………………………………………………………………………………………………

(e) Yakinisha sentensi ifuatayo (alama 2)

Hakuwapiga wala kuwalaghai.

……………………………………………………………………………………………………………………

(f) Eleza viambishi katika neno lifuatalo (alama 3)

Walichokilalia

……………………………………………………………………………………………………………………

(g) Bainisha vivumishi vilivyo katika sentensi ifuatayo: (alama 2)

Wanafunza wote wenye nidhamu watapewa tuzo kubwa na mwalimu wao.

……………………………………………………………………………………………………………………

(h) Changanua sentensi ifuatayo ukitumia mistari au mishale (alama 4)

Yohana na Otieno hucheza kandanda.

……………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………

***©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]***

………………………………………………………………………………………………………………………

(i)Andika sifa tatu zinazobainisha sentensi changamano. (alama 3)

………………………………………………………………………………………………………

(j)Geuza sentensi ifuatayo iwe katika usemi halisi. (alama 2)

Askari jela alimwuliza Kendi kama alidhani hapo ni kwao. Alimwamuru aende kwake mara moja.

………………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………………

(k) Toa mfano wa neno lenye muundo ufuatao wa silabi. (alama 1)

IK+KI+KI+KI

………………………………………………………………………………………………………………………

(l) Onyesha matumizi ya viakifishi vifuatavyo. (alama 2)

(i) kibainishi

………………………………………………………………………………………………………………………

(ii)parandesi

………………………………………………………………………………………………………………………

(m) Tumia neno –baya kama: (alama 2)

(i) kiwakilishi

………………………………………………………………………………………………………………………

(ii)kielezi

………………………………………………………………………………………………………………………

*©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]*

(n) Tunga sentensi sahili ukitumia kitenzi 'la' katika kauli ya tendewa. (alama 2)

.............................................................................................................................................

(o)Badlisha maneno yaliyopigiwa mstari yawe vitenzi. (alama 2)

Yunis amepata <u>faida</u> kutokana na <u>ukulima</u>.

.............................................................................................................................................

(p)Kwa kuzingatia maagizo andika upya sentensi ifuatayo: (alama2)

Tinga amewafanya ng'ombe wake wanywe maji.

(Anza kwa : Mifugo wangu …………..usitumie 'amewafanya')

.......................................................................................................................................

(q)Onyesha miundo miwili ya nomino za ngeli ya U-U. (alama 2 )

........................................................................................................................................

(r) Bainisha maana mbili zinazojitokeza kutokana na sentensi hii. (alama 2)

Umu alimwandikisha mkewe.

........................................................................................................................................

(s)Tunga sentensi katika wakati uliopo hali isiyodhihirika. (alama 1)

.......................................................................................................................................

**4.ISIMUJAMII** (Alama 10)

(a) Lahaja huainishwa katika makundi mawili. Yataje (alama 2)

.............................................................................................................................................

.............................................................................................................................................

***©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]***

(b) Eleza sifa zozote nne za lugha ya taifa. (alama 4)

.............................................................................................................................................

.............................................................................................................................................

.............................................................................................................................................

.............................................................................................................................................

.............................................................................................................................................

.............................................................................................................................................

.............................................................................................................................................

.............................................................................................................................................

(c )Tolea ushahidi namna nne kwamba Kiswahili ni lugha ya kimataifa. (alama 4)

.............................................................................................................................................

.............................................................................................................................................

.............................................................................................................................................

.............................................................................................................................................

.............................................................................................................................................

.............................................................................................................................................

.............................................................................................................................................

............................................................................................................................................

*©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]*

**JINA.................................................................................................NAMABARI...........**

**SHULE.................................................................................................TAREHE.................**

**DARASA.............................................................................................SAHIHI.......................**

**102/3**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 3**
**CLASS OF KCSE 2024**
**TIME: 2 ½ HOURS**

# THE RIFT VALLEY & NORTH EASTERN KCSE JOINT NATIONAL MOCK 2024

Kenya Certificate of Secondary Education (KCSE)

**MAAGIZO**

a) Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu
b) Jibu maswali manne pekee
c) Swali la kwanza ni la lazima
d) Maswali hayo mengine yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobakia yaani : Riwaya, hadithi fupi,ushairi na fasihi simulizi
e) Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja
f) Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili
g) Majibu yote sharti yaandikwe kwenye nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| USHAIRI | 20 | |
| TAMTHILIA | 20 | |
| RIWAYA | 20 | |
| HADITHI FUPI | 20 | |
| FASIHI SIMULIZI | 20 | |
| JUMLA | | |

*©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]*

**SEHEMU YA A:** ***Mapambazuko Ya Machweo Na Hadithi Nyingine- Clara Momanyi***

**SWALI LA LAZIMA**

**1.** "Mike! Mike! Mike! Njoo! Nilijua utafanya vyema mwanangu…"

(a) Tambua na ueleze **toni** ya dondoo hili. (alama 2)
(b) Changanua mtindo katika dondoo hili. (alama 2)
(c) Eleza sifa **nne** za msemaji wa dondoo hili. (alama 4)
(d) Eleza mbinu **mbili** ulizozitumia kutambua sifa za msemaji wa dondoo hili. (alama 4)
(e) Tambua na ufafanue madhila yanayomsakama mhusika mkuu katika hadithi hii ya *"Sabina"*. (alama 8)

**SEHEMU YA B: RIWAYA**

***Nguu Za Jadi***

***Jibu swali la 2 au 3***

**2.** Eleza umuhimu wa mandhari ya kanisa ukirejelea riwaya ya Nguu za jadi (al 20)

**3.** Fafanua maudhui ya ajira ya kazi yanavyojitokeza katika riwaya ya Nguu za Jadi (al 20)

**SEHEMU YA C: TAMTHILIA**

***Bembea ya Maisha- Timothy Arege***

***Jibu swali la 4 au 5***

**4**."…anachukua vidonge vyake na kuvimeza kabla ya kuketi kwenye kochi mpya."

(a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)
(b) Tambua aina za taswira katika dondoo hili. (alama 2)
(c) Eleza umuhimu wa mandhari ya dondoo hili. (alama 4)
(d) Eleza nafasi ya mwanamke ukijikita katika utamaduni wa jamii ya *"Bembea ya Maisha"*. (alama 10)

**AU**

**5**. " Wakati mwingine maisha haya hukufanya kijisikia kama abiria kwenye gari liendalo kwa kasi. Unatamani dereva apunguze mwendo lakini unakumbuka kuwa safari bado ni ndefu na hutaki kufika ukiwa umechelewa. Basi unatulia japo ndani una wasiwasi, hutulii. Lakini huwezi kushuka maana safari itaganda. Kwa hivyo, unajitahidi tena, japo wakati mwingine unajikuta umetambaliwa na uchovu, shaka na tuhuma."

***©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]***

(a) (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
(b) Changanua mtindo katika dondoo hili. (alama4)
(c) Dhihirisha umuhimu wa mzungumziwa wa maneno haya katika kuijenga tamthilia ya *"Bembea ya Maisha*". (alama 6)
(d) Eleza namna maisha yanamfanya mzungumzaji "kujisikia kama abiria kwenye gari liendalo kwa kasi".(alama 6)

**SEHEMU YA D: USHAIRI**
***Jibu swali la 6 au 7***

6. ***Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.***

Jama, Jama, Jamani
Mbona twabebeshwa mateso hivi
Mizigo mikubwa ya dhiki kama
Kwamba hatuna haki ya kusema
Kukataa ndoa za lazima
Kukataa kuozwa wazee
Kukataa kukatishwa masomo
Kukataa tohara ya lazima

Jama, Jama Jamani
Iweje tuteswe mateso haya
Na watu wasio kuwa hata na haya kama
Kwamba hatuna haki ya kulalamika
Kulalamikia kutumikishwa kama mayaya
Kulalamikia kudhalilishwa kiunyama
Kulalamikia kutolindwa na sheria

Jama, Jama, Jamani

Sasa hii ni awamu nyingine

Na macho tumeyafungua kabisa

Tumekataa kudhalilishwa kabisa

Tumekataa kuteswa kama watumwa

Tumekataa tohara ya lazima

Tumekataa kuozwa....... Tumekataa! Tumekataa

Hii awamu ya 'Haki ya mtoto wa kike'

**<u>Maswali</u>**

(a) Taja mambo **matatu** muhimu yaliyozungumziwa na mshairi kisha ueleze kila moja . (alama 6)

(b) Eleza muundo wa shairi hili (alama 4)

(c) Taja mbinu **mbili** za lugha alizotumia mshairi kisha ueleze kila moja (alama 4)

(d) Kwa nini mshairi huyu anasema hii ni 'awamu' nyingine? (alama 3)

(e) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa na mshairi (alama 3)

(i) awamu

(ii) kudhalilishwa

(iii) Dhiki

**AU**

**7. <u>Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo</u>**

1. Mkata ni mkatika, harithi hatoridhiwa
Sina ninalolishika, wala ninalochukuwa
<u>Mlimwengu</u> <u>kanipoka,</u> hata tone la muruwa!
Mrithi nini wanangu?

2. Sina ngo'mbe sina mbuzi, <u>sina konde sina buwa</u>
Sina hata makaazi, mupasayo kuyajuwa
Sina mazuri makuzi, jinsi nilivyoachwa
Mrithi nini wanangu?

*©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]*

3. Sina kazi sina bazi, ila <u>wingi wa shakawa</u>
Sina chembe ya majazi, mno nikukamuliwa
Nakwa'cheni upagazi, ngumu kwenu ku'tuwa
Mrithi nini wanangu?

4. Sina sikuachi jina, mkata hatasifiwa
Hata nifanye la mana, mno mi kulaumiwa
Poleni wangu sana, sana kwenu cha kutowa
Mrithi nini wanangu?

5. Sina leo sina jana, sina kesho kutwaliwa
Sina zizi sina shina, wala tawi kuchipuwa
Sina wanangu mi sina , sana la kuacha kuraduwa
Mrithi nini wanangu?

6. Sina utu sina haki, mila yangu meuliwa
Nyuma yangu ili dhiki, na mbele imekaliwa
N'nawana na miliki, hadi nitakapofukiwa
Mrithi nini wanangu?

7. Sina ila kesho kwenu, wenyewe kuiongowa
Muwane kwa nyinyi mbinu, mwende pasi kupumuwa
Leo siyo kesho yenu, kama mutajikamuwa
Mrithi nini wananngu?

(a) Taja mambo yoyote **mawili** ambayo mtunzi angewarithisha wanawe. (alama 2)

(b) Eleza sababu ya mtunzi kutoweza kuwarithisha wanawe. (alama 3)

(c) Andika ubeti wa nne kwa lugha nathari. (alama 4)

(d) Dondoa mifano **miwili miwili** ya : (alama 2)

(i) Inkisari

(ii) Tabdila

(e) Chambua shairi hili kwa upande wa :

(i) Dhamira (alama2)

(ii) Muundo (alama 4)

(f) Eleza maana ya vifungu vifuatavyo kama vilivyotumiwa katika shairi. (alama 3)

(i) Mlimwengu kanipoka

(ii) Sina konde sina buwa.

***©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]***

(iii) Wingi wa shakawa.

## SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI

**8. Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali.**

Malaika
Nakupenda malaika x2
Ningekuoa malaika...
Ningekuoa dada...
Nashindwa na mali sina wee...

Ningekuoa malaika x2

Pesa, zasumbua roho yangu x2
Nami niafanyeje, kijana mwenzio
Nashindwa na mali sina wee...

Ningekuoa malaika x2

(a) Ainisha wimbo huu kwa kuzingatia kipengele cha maudhui. (alama 2)
(b) Andika sifa **mbili** za jamii inayosawiriwa na wimbo huu. (alama 2)
(c) Eleza mikakati **sita** ambayo mwimbaji angetumia kufanikisha uwasilishaji wa wimbo huu. (alama 6)
(d) Unanuia kutumia mahojiano kukusanya habari kuhusu nyimbo za aina hii.
 (i) Eleza manufaa **matano** ya kutumia mbinu hii. (alama 5)

 (ii) Eleza changamoto **tano** za kutumia mbinu hii. (alama 5)

*©KNEC 2024 [Contact 0724333200 for Marking Schemes or Order online at www.kenyaeducators.co.ke]*